

# KUTAYARISHA BAJETI KWA MTAZAMO WA KIJINSIA

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)

Kimechapishwa na
**MTANDAO WA JINSIA TANZANIA (TGNP)**
S.L.P. 8921
Dar es Salaam
Tanzania

Usanifu: Petra's Maridadi Ltd.
Katuni ya Jalada: Zumba Pius Malili

© TGNP, 2000
Haki zote zimehifadhiwa.

ISBN: 9987-600-14-X

# Yaliyomo

*Dibaji* v

**SURA YA KWANZA:** UTANGULIZI 1
Kuhusu Kitabu Hiki 1
Bajeti ni Nini? 3
Bajeti ya Kijinsia 5
Kwa Nini Tanzania Inahitaji Bajeti ya Kijinsia 6
Jinsi Utafiti Ulivyofanyika 10
Tunapaswa Kushinikiza Nini? 11

**SURA YA PILI:** TUME YA MIPANGO NA WIZARA YA FEDHA
Bajeti ya Serikali ni Nini? 13
Mabadiliko Katika Bajeti ya Serikali 16
Wanawake na Wanaume Katika Uchumi wa Tanzania 18
Ni Nani Anayetayarisha Bajeti ya Serikali? 19
Hitimisho 22

**SURA YA TATU:** SEKTA YA AFYA 23
Watu Tofauti wana Mahitaji Tofauti ya Afya 23
Sera ya Afya Tanzania 26
Wahisani wa Nje na Mipango ya Uwekezaji Kisekta 27
Bajeti ya Afya 28
Hali ya Wafanyakazi wa Kike na Kiume Katika Afya 31
Wasichana na Wanawake na Bajeti ya Serikali ya Afya 32
Umma au Binafsi? 36
Ili Kutumia Zaidi Serikali Inahitaji Mapato Zaidi 36
Tunataka Mabadiliko Yapi Katika Bajeti ya Afya ya Serikali 38

**SURA YA NNE:** ELIMU 39
Utangulizi 39
Historia ya Elimu Tangu Uhuru 40
Bajeti ya Elimu 43
Shule za Msingi 44
Shule za Sekondari 46
Elimu ya Juu 48
Elimu ya Watu Wazima 51
Walimu 51
Mapato 52
Fedha Kutoka kwa Wahisani wa Nje 53
Ni Nani Mwenye Uwezo wa Maamuzi 55
Ni Nini Kitakachosaidia Kufanya Elimu Tanzania Kuwa Bora

# Dibaji

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni shirika lisilo la kiserikali lenye lengo la kuwezesha mchakato wa usawa wa jinsia, haki na uwezeshaji wa wanawake katika hatua tofauti kwenye jamii ya Watanzania. Tangu kuanzishwa kwake hapo mwaka 1993, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) umekuwa ukijishughulisha na mipango mikuu mitatu; Mafunzo na Kujenga Uwezo, Habari na Uenezi, Ushawishi na Utetezi wa masuala muhimu ya jinsia na maendeleo kwa ujumla. Uchambuzi wa kijinsia katika hatua tofauti za utekelezaji wa programu mbalimbali, mbinu za ushirikishaji na za kusisimua, kuibua mambo, ujenzi wa kuungana na wa kutandaa,vyote vimekuwa ni baadhi ya mbinu zilizotumiwa kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Kwa kupitia Programu ya Kushawishi na Kutetea, Mtandao na vyama vishiriki husùsan katika uhamasishaji wa haki na usawa wa wanawake kwa kupitia Mtandao wa wanaharakati (FemAct), wamekuwa wakishirikiana kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili na nusu, wakifuatilia mchakato mzima wa mipango kitaifa na ugawaji wa rasilimali, au bajeti ya taifa. Mkazo umekuwa kuchunguza jinsi michakato hiyo imekuwa na athari hasa kwa wanawake (wakiwemo watoto wa kike) pamoja na makundi mengine yaliyosahaulika kama vile wanaume maskini, vijana na wazee.

Katika mwaka 1997 kwa kupitia Tamasha la Mafunzo ya Jinsia (AGSC '97), TGNP ilizindua Mpango wa Bajeti ya Kijinsia (GBI) ambao ni Mpango unaolenga katika kuleta mabadiliko ya usawa kijinsia, katika sera za kiuchumi nchini na unaolenga kwa ujumla katika mkazo na michakato ya bajeti ya taifa pamoja na athari yake kwa makundi tofauti ya watu (wanawake, wanaume na vijana). Ikiwa ni sehemu ya mchakato

huu muhimu, utafiti wa michakato ya kibajeti kwa kiwango kipana pamoja na ugawaji wa rasilimali uliendeshwa katika wizara nne muhimu. Wizara hizo ni: Tume ya Mipango na Wizara za Fedha, Elimu na Afya. Utafiti ulilenga katika kuchambua sekta hizi na kutambua mapungufu ya kijinsia yaliyopo katika michakato ya kupanga na kutayarisha bajeti pamoja na athari za michakato hii kwa makundi mbalimbali nchini. Sekta nne zilichaguliwa kama sehemu za muhimu za mwanzo, mbili zikiwa muhimu kwa kiwango cha taifa cha mgawo wa rasilimali na nyingine mbili zikiwa muhimu katika kuamua hali njema ya Watanzania wote, wanawake na wanaume, watu wazima na watoto.

Shabaha ya Bajeti ya Kijinsia siyo kuwa na bajeti tofauti ya wanawake nchini, bali ni kushawishi bajeti ya taifa na michakato yake ya kibajeti kukubali uchambuzi wa kijinsia utakaoweza kuwafikia na kuwanufaisha jinsi zote (wanawake na wanaume) kwa misingi iliyo sawa zaidi. Katika nchi hii kama zilivyo nchi nyingine nyingi, bajeti za taifa na michakato ya kibajeti imekuwa na historia na mitazamo ambayo inaweka pembezoni mahitaji ya baadhi ya watu hususan wanawake, wanaume maskini na vijana. Matokeo yake ni kuwa makundi haya yamefaidika kidogo sana kutoka kwa mipango ya taifa na mgawo wa rasilimali yaani bajeti ya taifa.

Chapisho hili limeenezwa kwa watu kwa kutumia lugha rahisi na yenye sentensi fupi na nyepesi kuhusu matokeo makubwa ya utafiti wa bajeti ya kijinsia ulioendeshwa katika sekta nne zilizotajwa hapo juu. Chapisho lina sura nne. Sura ya kwanza ni utangulizi unaoweka sawa mfumo na dhana mbalimbali za mpango wa bajeti ya kijinsia na kufafanua dhana muhimu zilizotumiwa katika kitabu. Pia kimeweka sawa sababu za msingi, kwa nini bajeti ya kijinsia? Sura ya pili inaeneza dhima ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha katika suala zima la mipango

mikubwa ya kiuchumi na mgawo wa rasilimali. Vilevile uwezo mkubwa walionao vyombo hivi katika kugawa rasilimali za taifa kupitia bajeti za taifa. Mapungufu ya kijinsia yaliyogunduliwa katika sekta hizi ni utambuzi muhimu sana unaohitaji uwiano zaidi wa jinsia katika mipango mikubwa ya kiuchumi na kutayarisha bajeti. Sura ya tatu inaeneza matokeo muhimu ya utafiti katika sekta ya Afya. Mapungufu ya kijinsia katika huduma za afya zinazopata rasilimali kidogo hasa zile ambazo zinahusika na dhima za kibiolijia za wanawake (na hatari zinazoambatana nazo), hatari za kiafya kutokana na kazi, huduma hafifu katika vituo vya afya ni baadhi ya masuala yaliojadiliwa katika sura hii. Masuala mengine muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na athari hasi ya uchangiaji wa gharama hususan wazee, wanawake, wajawazito katika ngazi ya taifa na kijiji. Sura ya mwisho ni juu ya sekta ya Elimu. Sura hii inaeleza jinsi mifumo ya Elimu ilivyozorota nchini iliyosababishwa na kupatiwa rasilimali kidogo kwa sekta hii muhimu hasa wakati wa miaka kati ya 1980 na 1990. Hii imeathiri mno wanawake na watoto wa kike wakiwa hawana vifaa vya kuwawezesha kushindana na wenzao wa kiume katika nyanja mbalimbali. Watanzania sasa wanashuhudia limbikizo la deni la kutokujua kusoma miongoni mwa wanawake, wazee,vijana na kizazi kijacho. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Shirika la UNICEF, zaidi ya asilimia 50% ya watoto nchini wanaotakiwa kwenda shule hawaendi shule.

Kitabu hiki pendwa ni matokeo ya michango ya watu binafsi na hasa washiriki wa mtandao wa mashirika ya kutetea haki na usawa kwa wanawake (FemAct) na taasisi nyingine. Kwa kuwa haitawezekana kuwataja wachangiaji wote kwa majina, Mtandao ingependa kutambua na kukiri michango yote na misaada iliyotolewa wakati wa maandalizi na kitabu kwa kuwataja wachache ndani ya TGNP/FemAct na kuwashukuru watafiti

wote walioshiriki katika utafiti wa awali, wahariri na wapitiaji waliotumia muda wao kuwezesha kitabu hiki kisomeke. Hususani Mtandao ungependa kushukuru ushauri wa kiufundi na maelekezo ya Prof. Ruth Meena wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ms. Debbie Budlender wa Afrika Kusini, ambao walitoa wakati wote wa matayarisho ya kitabu hiki. Mtandao pia unatoa shukrani kwa ndugu Stephen Maina kwa tafsiri hii ya Kiswahili.

Hali kadhalika, Mtandao ungependa kuwashukuru Ubalozi wa Uholanzi Tanzania kwa msaada wa kifedha kwa programu ya GB1 katika muda wa miaka miwili na nusu na misaada ya kitaasisi iliyotolewa na shirika la Konrad Adeneuer Foundation (KAF) kwa kipindi cha miaka mitano sasa.

Mwisho Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ungependa kutambua ushirikiano uliotolewa na vyombo mbalimbali vya habari nchini, hususan uongozi wa magazeti ya *The Guardian Limited* na *The Daily Mail* kwa kukubali kwao kwa vichwa vya habari na picha zilizochapishwa kwenye kitabu hiki. Kwa wote Wana Mtandao wanasema 'Ahsante'.

**Kuhusu Kitabu Hiki**


Kitabu hiki kinahusu bajeti ya serikali. Kinaangalia Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango. Vyombo hivi viwili vinaelekeza wizara nyingine za serikali jinsi wanavyopaswa kutayarisha bajeti zao. Kinaangalia pia bajeti za serikali katika sekta za Elimu na Afya. Afya na Elimu ni huduma mbili muhimu mno ambazo serikali inawajibika kutoa kwa watu wake, hasa wanawake, vijana na wanume maskini.




*Hii ni kauli nzuri ya Waziri wa Fedha, juu ya uwajibikaji wa serikali. Hata hivyo ni taratibu zipi zilizopo zinazohakikisha kuwa sekta za kijamii zinafaidika nchini kutokana na unafuu wa ulipaji madeni?*

Kwa ujumla, Bajeti inasema jinsi serikali inavyopanga kutumia fedha zake kwa mwaka ujao. Inasema pia ni wapi na kwa namna gani serikali itapata fedha zake. Kitabu hiki kinaangalia jinsi fedha za serikali zinavyotumika na huduma zinavyotumia fedha na athari zake kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Kinaangalia pia ni nani anayefanya maamuzi haya muhimu sana kuhusu mambo haya.

Wanawake na Wanaume ni tofauti kwa sababu miili yao ni tofauti.Tunaziita hizi ni tofauti za kibaiolojia. Wanawake na Wanaume pia ni tofauti kwa sababu wanafanya majukumu tofauti. Wanawake wanazaa watoto, wanawanyonyesha, wanawatunza na




wanawafundisha. Wanawake wanafanya kazi nyingi za kutunza na kusafisha nyumba, kuchota maji na kutafuta kuni, kupika na kuangalia mahitaji mengine ya familia.


Hasa huko vijijini, wanawake wanafanya pia kazi mashambani kulima na kuhakikisha chakula cha familia kinapatikana. Mara nyingi hawalipwi kwa kufanya kazi hizi. Na serikali haijaanza kujumlisha kazi hizi wakati wanakokotoa ukubwa wa uchumi kupitia vipimo vya Jumla ya Pato la Ndani (GDP).

Mara nyingi wanaume wanafanya kazi nje ya nyumbani kwao. Kwa mfano wanauza vitu na kutengeneza vitu. Wanaume wengi wanalipwa kwa kazi wanazofanya. Pia sehemu kubwa ya kazi za wanaume zinaingizwa katika GDP. Kwa namna hii, mara nyingi mchakato wa GDP hauonyeshi mchango wa wanawake katika uchumi wa taifa. Hata hivyo, pato la ndani la uchumi nchini huonyesha kuwa wanawake na wanaume wa Tanzania ni masikini. Lakini wanawake ni masikini zaidi kuliko wanaume. Kazi nyingi wanazofanya hawalipwi. Wengi ni masikini kwa sababu mila na sheria haziwaruhusu kumiliki mali. Vilevile ni masikini kwa sababu ndani ya familia zao wanaume wanaudhibiti zaidi kuliko wanawake juu ya fedha na maamuzi kwa wanawake na wanaume

ni tofauti. Mara kadhaa wanakuwa na mahitaji tofauti. Kitabu hiki kinaangalia kama matumizi ya serikali yanakidhi mahitaji haya tofauti. Kinaangalia pia kama matumizi ya serikali yanawasaidia wanawake na wanaume kuwa sawa.

**Bajeti ni Nini?**


Tanzania ni nchi masikini. Haina fedha za kutosha kugharamia mahitaji yote ya watu wake wote mara moja. Serikali lazima ichague ni wapi itatumia fedha zake. Ni lazima ichague ni mambo yapi ni ya muhimu na ya haraka. Tunayaita mahitaji haya 'Vipaumbele'.


Tanzania reducing army expenditure — Minister

*'Ikiwa ni nchi maskini Watanzania wengi wangependa kuona kauli kama hii inatekelezwa'.*

Serikali ina sera zinazosema vipaumbele vyake ni nini. Kwa mfano, ina Sera ya Afya, Sera ya Elimu, Sera ya Kilimo na kadhalika. Sera zinasema ni nini Serikali inataka kufanya ili ifanye Tanzania iwe ni mahali pazuri zaidi kwa watu wake. Bajeti inasema ni wapi serikali itatumia fedha zake ili kufanikisha mambo hayo. Kwa kuwa hazipo fedha za kutosha kwa kila kitu, serikali lazima ichague. Inapaswa kuchagua ni kiasi gani cha fedha kitatolewa kwa sekta za Afya, Kilimo, Maji, na kadhalika. Halafu inapaswa kuchagua jinsi ya kutumia fedha ndani ya Wizara za Elimu, Kilimo na wizara nyingine zote. Bajeti ni muhimu sana kwa sababu bila fedha, wizara hazitaweza kufanya kazi zake kikamilifu.

Serikali vilevile lazima iamue kiasi gani cha fedha inahitaji kukusanya na itakusanya wapi. Kiasi kikubwa cha fedha za ma-




pato kinatoka kwa raia wa Tanzania. Kwa mfano, raia wanaume na wanawake wanaipa serikali fedha kupitia kodi, ushuru na kwa kulipia huduma kama vile karo, kodi ya maji na kadhalika. Kiasi kingine cha fedha kinatoka kwa wahisani nje ya nchi. Sehemu ya fedha hizi kutoka nje zinakopwa na serikali lazima ilipe deni hili baadaye.

Watanzania wote wana haki ya kushiriki katika maamuzi ya bajeti iweje. Zaidi ya miaka mia moja iliyopita, wakati watu wa Ulaya walipoanza kupigania haki ya kupiga kura na kuwachagua viongozi, wito wao mkubwa ulikuwa 'Hakuna kodi bila uwakilishi'. Walikuwa wakisema kuwa hawakutaka kutoa fedha serikalini hadi hapo watakapochagua watu watakaoshiriki katika kuamua jinsi fedha hizo zitakavyotumika.

Katika nchi nyingi, wanaume walipata haki ya kupiga kura muda mrefu kabla ya wanawake. Wanawake iliwabidi washinikize kwa muda mrefu zaidi ili wasikike na kupata haki hizo. Kitabu hiki kitaonyesha kuwa vita vya ushinikizaji wa masuala ya haki za wanawake bado havijaisha. Kwa mfano, mara nyingi bado ni wanaume ambao wanafanya maamuzi muhimu juu ya bajeti ya taifa. Kwa kuwa wizara haziwezi kufanya yale

wanayotaka kufanya bila fedha, wanaume ambao wao ndio watungasera na wapangaji bajeti hawa wanafanya maamuzi juu ya nini serikali inafanya.




*Hakuna kipya wala mwelekeo katika bajeti nyingi na michakato ya bajeti ya serikali. Mambo mengi yanahitajika kufanyika ili mahitaji ya makundi yaliyowekwa pembezoni, hasa wanawake na watoto wanakuwemo kwenye bajeti.*



**Bajeti ya Kijinsia**

*Jinsia* ni neno tunalotumika kueleza tofauti za mahusiano kati ya wanawake na wanaume. Mahusiano haya hujengwa na jamii, na bahati mbaya mara nyingi hayalingani. Bajeti ya kijinsia ni bajeti ambayo inatoa haki kwa wanawake na wanaume. Ili kuwa na bajeti ya kijinsia, watu wanaotayarisha bajeti lazima wafahamu juu ya tofauti za kibiolojia na tofauti nyingine kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Wanapaswa kugawa fedha kwa njia ambayo itawasaidia wanawake na wanaume, wasichana na wavulana kuwa na usawa zaidi kwenye jamii. Kwa uhakika, wanapaswa kupunguza 'mapungufu ya kijinsia' yanayojitokeza nchini na ndani ya jamii yawe madogo zaidi.


Bajeti ambayo haiangalii masuala ya jinsia itakuwa ina mapungufu. Kama serikali haiwasaidii wanawake kufanya kazi zao za kila siku kwa kuwaongezea rasilimali ya mahitaji yao, hawatafanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi. Watakuwa pia na muda mdogo wa kujipatia fedha na familia zao. Kama serikali itawasaidia wanawake kwa kusogeza maji karibu na nyumba zao, kwa kuwaelimisha, kwa kuwasaidia kuwalelea watoto, kwa kugharamia vituo vya mafunzo ya awali, wanawake na nchi nzima watafaidika. Nchi haiwezi kufanya kazi kwa ufanisi kama nusu ya wananchi wake, yaani wanawake ni lazima wapambane na mazingira magumu ili wafanye kazi zao za kila siku.

Dhana kuu hapa ni; Bajeti ya kijinsia siyo bajeti maalumu kwa ajili ya wanawake pekee bali bajeti ya jinsia ni njia ya kugawa bajeti yote ya serikali kwa haki na ufanisi zaidi.

**Kwa Nini Tanzania Inahitaji Bajeti ya Kijinsia**

Tangu uhuru, Tanzania imekuwa na sera zinazoongelea kuhusu usawa wa wanawake na wanaume. Kwa mfano, tangu uhuru Tanzania imekuwa na sera zinazosema kuwa wananchi wote wanapaswa kufurahia afya na elimu na kuishi maisha mazuri.

Leo hii bado wako Watanzania ambao hawajapata mambo haya ili kukidhi mahitaji yao kwa kina. Na bado kuna tofauti kubwa ya kutokuwa na usawa kati ya wanawake na wanaume.




Baadhi ya tofauti hizi kati ya wanawake na wanaume ni za kibaiolojia. Lakini sehemu kubwa ya kutokuwa sawa inakuzwa na watu mbalimbali kwenye jamii, wakiwemo wale watengeneza sera na bajeti ya taifa. Mara nyingi, kutokuwa sawa kunatokea kwa sababu wanawake wana

uwezo kidogo kuliko wanaume. Wana uwezo mdogo katika familia zao ambako wanaume wanadhibiti fedha na mambo mengi. Wana uwezo mdogo nje ya familia zao ambako wanaume tena wanafanya maamuzi muhimu, hasa yanayohusu sera za taifa.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni shirika lisilo la kiserikali. Tangu mwaka 1993 TGNP imekuwa ikifanya kazi kuifanya Tanzania mahali pa usawa zaidi kwa wanawake na wanaume. TGNP inafahamu kuwa maamuzi yahusuyo sera za mipango mikubwa ya kiuchumi na bajeti ni baadhi ya maamuzi muhimu hapa nchini. Maamuzi haya yanaweza kuwafanya wanawake na wanaume wasiwe na usawa au yanaweza kuwasaidia wawe sawa zaidi. Ni kutokana na sababu hii Mtandao na washiriki wake umeamua kufanya utafiti kuhusu bajeti ya kijinsia nchini.

Tanzania siyo nchi ya kwanza kuwa na mpango wa bajeti ya kijinsia. Serikali ya Australia ilianza bajeti ya kijinsia katikati ya miaka ya 1980. Huko Afrika ya Kusini, mashirika yasiyo ya kiserikali na wabunge walishirikiana na kuanzisha bajeti ya wanawake hapo mwaka 1995, mara baada ya kumalizika kwa ubaguzi.

Tanzania inaweza kujifunza kutoka katika bajeti za kijinsia za nchi nyingine. Lakini bajeti ya kijinsia ya Tanzania itakuwa tofauti kwa sababu nchi yetu ni tofauti na nchi nyingine. Bajeti ya kijinsia ya Tanzania inapaswa kuangalia kwa mfano, umasikini tangu miaka ya mwanzo ya Ujamaa. Bajeti ya kijinsia Tanzania inapaswa kuangalia jinsi sera za Ujamaa kama vile elimu ya msingi kwa wote (UPE) na huduma ya Afya ya msingi kwa wote (UPHC) ilivyosaidia watu masikini na kusaidia kupunguza mianya kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Inapaswa kuangalia ni nini kilichobadilika tangu sera hizi zilipobadilishwa. Sera kuhusu Afya na Elimu katika kitabu hiki zitaeleza sehemu ya taarifa hii. Mabadiliko mengi tangu Ujamaa yamefanya mambo yawe magumu hasa kwa wanawake na

wanaume masikini. Lakini baadhi ya mabadiliko yalikuwa mazuri. Kwa mfano.

Watanzania wanazungumza zaidi sasa kuhusu demokrasia. Wanasema kuwa serikali ni lazima iwasikilize wanawake na wanaume wa kawaida na kutoa ripoti kwa wananchi wa kawaida. Bajeti ya Kijinsia ni sehemu ya mabadiliko haya. Inasema kuwa serikali ni lazima ituarifu juu ya matumizi ya fedha zetu, na nini mipango yake katika kuyafanya maisha ya wananchi yawe bora zaidi, na hasa kukidhi mahitaji ya wanawake na wanaume, ya vijana na wazee nchini.

Leo tunaishi katika dunia ambako kuna mahusiano mengi kati ya nchi zetu. Kunakuwepo na mahusiano wakati watu wanapotembeleana na wakati vitu vinapotembea. Kwa mfano, wakati watu wa nchi moja wanapouza bidhaa kwa watu wa nchi nyingine. Mahusiano haya yanamaanisha kuwa kinachotokea katika nchi moja kinaathiri nchi nyingine nyingi.

Mapema katika miaka ya 1990 dunia imebadilika wakati Umoja wa Kisovieti na nchi nyingine za Ulaya ya Mashariki ziliposambaratika. Nchi hizi zilikuwa za ujamaa. Kama ilivyokuwa Tanzania, nchi ya ujamaa. Nchi hizi ziliamini kuwa serikali haina budi kutekeleza mahitaji muhimu ya wananchi. Baada ya kusambaratika, zilibadilisha msimamo wao.

Leo hii katika nchi zote, serikali zinafanya mambo machache katika kutoa huduma kwa wananchi kuliko zamani. Badala yake, serikali nyingi zinasema kwa njia bora zaidi kwa nchi kuendelea ni kwa kampuni binafsi kukidhi mahitaji mengi inavyowezekana. Wanasema kuwa kampuni binafsi zitafanya kazi vizuri zaidi na kwa ufanisi kwa sababu zinataka kupata faida. Mabadiliko ya kiuchumi kutoka serikalini na kuwa katika kampuni binafsi yanaitwa **biashara huria**.


Biashara huria haijaweza kuzisaidia nchi zote kwa usawa. Nchi nyingi za Afrika zimekuwa masikini zaidi kuliko mwanzo zilivyokuwa. Kwa mfano hapa nchini bidhaa tunazonunua kuto

ka nchi nyingine zimekuwa ghali zaidi. Wakati huo huo bei ya bidhaa wanazopata Watanzania kwa chakula imeshuka. Mwanya kati ya nchi tajiri na masikini umekuwa mkubwa. Baadhi ya nchi tajiri zaidi mara kadhaa zimesaidia nchi masikini kama Tanzania. Zinatoa msaada moja kwa moja au kupitia mashirika kama vile Benki ya Dunia na Mfuko wa Kimataifa wa Fedha (IFM). Tanzania inahitaji msaada huu kwa sababu bajeti yake ni ndogo sana. Lakini nchi tajiri na mashirika yatatoa misaada kama Tanzania itakubali kubadili sera zake.

Chini ya ujamaa, serikali iliwania kugharamia mahitaji karibu yote ya wananchi wa Tanzania. Leo, kwa sababu serikali ina fedha kidogo na kwa sababu ya wahisani wengi wanavyosema duniani, serikali inazungumza juu ya kufanya kazi pamoja na kampuni binafsi ya nje na ndani ya nchi na kwamba wananchi wa kawaida kugharamia mahitaji yao, yaliyo mengi.

Kugharamia mahitaji yake, inazungumzia pia kuhusu kazi za wanawake na wananchi wengine maskini. Ni wanawake wanaoelimisha, kulisha na kuwatunza wagonjwa wakati serikali haifanyi hivyo. Hii inaongeza katika kazi ambazo hazilipwi na taifa.

Wakati serikali walipopunguza matumizi, punguzo kubwa zilitoka katika sekta za afya na elimu. Uamuzi huu una madhara yake, hasa kwa wanawake na makundi mengine masikini. Ndiyo maana Mtandao wa Jinsia na washiriki wake waliamua kuzichunguza Wizara hizi katika programu yao ya kwanza ya bajeti ya kijinsia.



*'CCM itatumia sh. 500m/=, NCCR itapata ruzuku ya sh. 413m/= uchaguzi Bunda, Ubungo, Temeke utagharimu sh. 500m/= n.k. Kwa upande mwingine hakuna fedha za kuwarudisha shuleni wasichana wajawazito, hakuna fedha kwa elimu ya uraia ili watu wafahamu haki zao za kiraia!' Je , hii ndiyo bajeti wananchi wanayotaka?*

Wakati huduma za afya zinapunguzwa, watoto wengi na wachanga wanakufa na watu wanakuwa dhaifu. Wanawake wanafanya kazi nyingi zaidi kwa hao walio dhaifu na wagonjwa.

Wakati matumizi ya elimu yanapokatwa, watoto wachache na watu wazima hasa wanawake, wataweza kupata maarifa na stadi muhimu. Watu wenye elimu ndogo wanapata fedha kidogo na wanaishi katika hali duni. Watu wenye elimu kidogo wana uwezo kidogo katika jamii kwa sababu hawawezi kupata nafasi za juu. Wakati fedha zinapokosekana, familia mara nyingi wana-chagua kuwaelimisha watoto wao wa kiume badala ya watoto wa kike.

**Jinsi Utafiti Ulivyofanyika**

Watu wengi walisaidia kufanya utafiti kwa ajili ya kitabu hiki. Baadhi ya hao waliosaidia wametoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baadhi wametoka serikalini. Watu kutoka serikalini, Chuo Kikuu na mashirika yasiyo ya kiserikali wana uzoefu na maarifa tofauti. Utafiti huu una nguvu kwa sababu watu kutoka mahali mbalimbali walifanya kazi pamoja. Kwa mfano, watu kutoka serikalini waliwasaidia watafiti wengine kuelewa vizuri zaidi jinsi serikali inavyofanya kazi.

Wafanyakazi serikalini wanafahamu undani wa serikali kwa sababu wanafanya kazi hapo kila siku. Watu kutoka Chuo Kikuu na mashirika yasiyo ya kiserikali waliwasaidia watafiti wa serikali-ni kuelewa zaidi juu ya dhana ya jinsia, tofauti kati ya wanawake na wanaume na mahitaji yao kibajeti. Kufanya kazi kwa pamoja

katika utafiti kulikuwa ni msingi mzuri wa kuanzishwa kwa kufanya kazi pamoja kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali na serikali na baadaye kubadilisha bajeti ili ikidhi haja ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana wa Tanzania.

Watu wengi nchini hawaelewi masuala ya bajeti na hivyo huiogopa. Kwa watu wengi bajeti ni orodha ya tarakimu kubwa. Watanzania wengi hawajiamini kuhusu kufanya kazi na tarakimu. Kama wanawake na wanaume wanataka kushinikiza mabadiliko ya kijamii, ni muhimu kwamba waache woga huu.

Wakati wa utafiti, TGNP ilipanga mrejesho wa matokeo ya utafiti. Mrejesho huu ulifanyika kwa njia za warsha kwa wahusika wakuu, serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali n.k. Katika warsha hizi watafiti waliwaarifu washiriki yale waliyogundua.Washiriki walizungumza juu ya matokeo ya utafiti. Walitoa mawazo yao kuhusiana na utafiti juu ya bajeti. Maoni yao yaliwasaidia watafiti kuendelea na utafiti huu. Wakati huo huo washiriki walijifunza mambo mengi kuhusu bajeti na jinsia.

Mtandao wa Jinsia Tanzania unatumaini kuwa utafiti pamoja na kitabu hiki vitasaidia wanaume na wanawake kuelewa zaidi juu ya bajeti na jinsi fedha za nchi zinavyotumika. Kama wanawake na wanaume wanayaelewa mambo haya, wanaweza kuhakikisha kuwa wabunge wao watayasukuma mabadiliko haya na kwamba maofisa wa serikali watayafanya mabadiliko haya. Kwa namna hii wataweza kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kuwafanya wanawake na wanaume wa Tanzania wawe na usawa zaidi.

**Tunapaswa Kushinikiza Nini?**


Kitabu hiki kinahusu zaidi namna tunavyotaka bajeti ya serikali kubadilika ili iweze kusaidia wanawake na wanaume wote masikini na kuwasaidia wanawake na wanaume kuwa na usawa zaidi. Kitabu hiki kinaonyesha jinsi bajeti ya serikali inavyoweza kutumika vizuri zaidi kufanikisha mambo haya.

Tunafahamu kuwa Serikali siyo pekee inayowajibika kwa jinsi bajeti inavyoonekana. Mtandao inaelewa kwa nini serikali ya Tanzania haiwezi kila mara kukidhi haja za mahitaji ya watu kama inavyotaka. Tunafahamu kuwa Tanzania ni nchi masikini.

Tunafahamu kuwa wahisani mara nyingine wanataka Tanzania kufanya mambo ambayo serikali haingependa kufanya. Hapa inatubidi tuiunge mkono serikali kupigania.

- Fedha zaidi kutoka kwa wahisani,
- Fedha zaidi kama misaada badala ya mikopo,
- Bei ya juu zaidi kwa bidhaa Tanzania inazouza nje,
- Bei ya chini zaidi kwa bidhaa tunazonunua kutoka nje ya nchi.

Mabadiliko haya yote yatamaanisha kuwa Tanzania ina fedha nyingi zaidi za kutumia kukabili mahitaji yetu. Halafu tunapaswa kushinikiza kuona kuwa fedha za ziada zinazokuwepo nchini, zinatumika kwa njia nzuri.




**Tunapaswa kuhakikisha kuwa watu tajiri na makampuni yanasaidia na kuongeza fedha ambazo serikali inatumia kwa kulipa kodi zao na kutoa misaada.**

**Tunapaswa kuhakikisha kuwa fedha zinatumiwa kwa hao wanaozihitaji zaidi - wanawake na wanaume masikini wa Tanzania ambao hawana fedha za kutosha kwa mahitaji yao na ya familia zao.**

Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha huta-yarisha mipango yote na bajeti kwa ajili ya Serikali. Wanazieleza Wizara nyingine zote kiasi cha fedha kitakachotumika mwakani. Wizara zina-paswa kuamua kiasi kitakachotumia fedha hizi ili kutoa huduma kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wa Tanzania nchi nzima.

Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha wana uwezo mkubwa. Kama hawazingatii tofauti za mahitaji ya wanawake na wanaume wakati wa kuta-yarisha mipango na ugawanyaji wa rasilimali, itakuwa vigumu sana kwa wizara nyingine kufanya kazi zao kwa namna ambayo itawafanya wanawake na wanaume wawe na usawa zaidi.




Sura ya tatu na nne ya kitabu hiki zinaangalia bajeti za serikali katika Afya na Elimu. Sura hii inaangalia kwa jumla bajeti ya serikali ambayo inajumuisha wizara zote. Inaeleza bajeti ya serikali ni nini na sehemu zake tofauti ni zipi. Inaeleza jinsi bajeti ya serikali zilivyobadilika kuhusu njia tofauti ambazo wanawake na wanaume wamechangia katika uchumi wa Tanzania na jamii. Halafu inaonye-sha ni nani mwenye nguvu katika kuamua juu ya bajeti ya serikali.


**Bajeti ya Serikali ni Nini?**

Mwaka 1967 katika Azimio la Arusha, serikali iliahidi kupiga vita ujinga, maradhi na umasikini. Baada ya Azimio hili, serikali ilita-yarisha mipango ya maendeleo ya miaka mitano iliyolenga katika kutimiza ahadi hii. Leo, badala ya mpango wa miaka mitano, serikali

ina mpango wa miaka mitatu na bajeti ya mbele. Mpango huu unaonyesha ni kiasi gani serikali itaweza kutumia kila mwaka na kile ambacho kitatumia fedha hizo.

Bajeti ya serikali inaanza Julai mosi ya mwaka moja na kuishia Juni 30 ya mwaka mwingine. Kwa mfano, Bajeti ya serikali kwa mwaka 1997/1998 ilikuwa Tsh.695,300m/= Hii ina maana kuwa serikali imepanga kutumia kiasi hiki, lakini pia inabidi iseme ni wapi itapata kiasi hiki.

**Bajeti ya Serikali 1997/98**




*Jedwali 2.1:* **Bajeti ya mwaka 1997/98**

| **Matumizi** | **Tsh. (Millioni)** |
|---|---|
| Ya kawaida | 666,843 |
| Maendeleo | 308,796 |
| Jumla ya matumizi | 975,639 |
| | |
| **Mapato** | **Tsh. (Milioni)** |
| Kodi, Ushuru, n.k. | 695,300 |
| Misaada na Mikopo ya Nje | 340,034 |
| Toa: Malipo kwa Mikopo ya Ndani | (50,695) |
| Jumla ya Mapato | 975,639 |


*Tanbihi : Parandesi kwa ajili ya kulipa mikopo inamaanisha hiki ni kiasi cha kutolewa.*

Jedwali la 2.1 linaonyesha kuwa zaidi ya theluthi mbili za matumizi ya serikali kwa 1997/98 ni ya kawaida. Kwa upande wa

mapato, Bajeti inasema kuwa zaidi ya theluthi moja ya mapato ya serikali inatoka nje ya nchi. Watu wengi wanaotayarisha bajeti wanasema kuwa wao hawapendelei upande wowote wa jinsia. Wanasema kuwa bajeti zinazungumzia watu na hivyo hazibagui dhidi ya wanawake au wanaume kwa sababu watu wanajumuisha wanawake na wanaume.

Hii si kweli. Serikali inatumia fedha kutoa huduma kwa watu na watu hao ni wanawake, wanaume, wasichana na wavulana. Kama serikali ikitoa huduma nzuri za maji, kwa mfano, itawasaidia zaidi wanawake na wasichana wanaotumia saa nyingi kuchota maji kutoka kwenye mabwawa. Kama serikali ikijenga barabara na kuwaajiri wanaume tu kujenga barabara hizi, itawasaidia zaidi wanaume kuliko wanawake.

Kiasi kikubwa cha matumizi ya kawaida ya Bajeti ya Tanzania kinakwenda kulipa mishahara na ujira. Ni asilimia 40 tu ya watumishi wa serikali ni wanawake. Wanaume wanashika nafasi za juu. Nafasi hizi pia zinatoa mishahara ya juu. Kwa hiyo matumizi ya kawaida kwa ujira na mishahara yanawafaidi moja kwa moja wanaume kuliko wanawake.



Jinsi serikali inavyokusanya mapato inaweza pia kuathiri tofauti ya wanawake na wanaume. Kwa mfano, kodi kwa kampuni zitaathiri wanaume zaidi kuliko wanawake kwa sababu wako wanawake wachache sana wanaomiliki kampuni hapa Tanzania. Kodi ya mapato itaathiri pia wanaume kuliko wanawake kwa sababu wanaume wengi zaidi wanafanya kazi za kulipwa zenye viwango vikubwa vya kulipa kodi . Kodi kama vile kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni tofauti. Zitaathiri wanawake na wanaume na zitakuwa ngumu kwa wanawake na wanaume walio na kipato cha chini zaidi, ambao hupaswa kuchunguza kila shilingi inayokatwa kodi.

**Mabadiliko katika Bajeti ya Serikali yana Maana Gani kwa Wanawake na Wanaume Masikini?**

Tanzania ni nchi masikini. Baada ya Azimio la Arusha serikali ilijaribu kutoa elimu, afya na huduma nyingine kwa wananchi wote bure. Matatizo ndani ya nchi kama vile ukame na siasa katika Afrika ya Mashariki vilidhoofisha uchumi wa Tanzania. Uchumi ulivyokuwa dhaifu, serikali ikawa na fedha kidogo zaidi. Hivyo haikuweza kutoa huduma zote bila ya malipo. Kwa sababu Watanzania wengi wana kipato cha chini, kila mwaka serikali ilitumia fedha nyingi zaidi lakini ilipata mapato kidogo sana.

Kama alivyo binadamu, nchi haiwezi kuendelea kutumia fedha zaidi kuliko zinazoingia. Kuziba pengo kati matumizi na mapato, serikali hukopa fedha. Kuanzia katikati ya miaka ya 1980 Mfuko wa Kimataifa wa Fedha (IMF) na Benki ya Dunia, wakopeshaji wawili wakubwa kwa nchi masikini, walianza kukopesha fedha serikali ya Tanzania. Baadhi ya nchi za nje pia zilianza kukopesha au kutoa fedha kwa Tanzania.

Kukopa fedha kunaleta matatizo. Kwanza, kama alivyo binadamu, serikali inapokopa fedha ni lazima izirudishe kwa kiasi kile kilichokopa na kiasi cha nyongeza. Kiasi cha nyongeza


kinaitwa riba. Kila mwaka tangu mwaka 1986 riba iliyolipwa kwa mikopo imekuwa zaidi ya theluthi moja ya mapato yake ya ndani ya nchi.

Pili, IMF na Benki ya Dunia walisema kuwa watatoa fedha kwa Tanzania kama serikali itabadilisha mtindo wa utendaji kazi wake. Kwa mfano, walisema kuwa serikali lazima iajiri watu wachache zaidi. Wafanyakazi wachache kwa serikali kama vile walimu na manesi inamaanisha huduma mbaya kwa elimu na afya kwa wananchi wa Tanzania hasa walio masikini.

IFM na Benki ya Dunia vilevile walisema kuwa serikali haipaswi kudhibiti mashirika au kampuni nyingi. Badala yake iwaachie watu binafsi au kampuni za nje kuthibiti sehemu kubwa ya uzalishaji nchini. Badala ya kutoa huduma bure kwa wananchi, serikali haina budi kuziruhusu kampuni kutoa huduma kwa malipo. Kampuni zinataka kupata faida. Wanapata faida kwa kutoza ada. Hivyo mabadiliko haya yanamaanisha kuwa Watanzania wengi walianza kulipia huduma mbali mbali kama afya, elimu n.k. Kwa kuwa watu wengi masikini hawawezi kulipia gharama za huduma, leo kuna wanawake na wanaume wengi, wasichana na wavulana ambao hawawezi kupata elimu, afya na huduma nyingine wanazohitaji na wanazotaka.

Tatu, katika nchi masikini kama Tanzania, wako watu wachache matajiri wa kulipa kodi ya mapato. Hivyo kodi ya mapato inaweza tu kutoa kiasi kidogo cha mapato. Shirika la IMF na Benki ya Dunia wanasema kuwa serikali lazima itoze kodi kwa huduma inazotoa ili iweze kupata mapato. Serikali imeanza sasa kutoza ada kwa shule, hospitali na maji. Hii inafanya iwe vigumu kwa wanawake na wanaume masikini kupata elimu, afya na huduma nyingine wanazohitaji.

Wazo jingine kutoka IMF na Benki ya Dunia ni VAT ambayo ni Kodi ya Nyongeza ya Thamani . Kodi ya mapato inalipwa na watu na kampuni zinazopata kiasi fulani cha fedha. Wako watu wachache tu wanaopata kiasi hiki cha fedha. VAT inalipwa na




watu wanaonunua bidhaa. Kila mtu analipa VAT kwa sababu kila mtu ananunua kitu.

VAT ilianzishwa hapa Tanzania katikati ya miaka 1998. Hapa TanzaniaVAT inaongeza asilimia 20 kwa bei tunayolipa tunaponunua vitu. Katika nchi nyingine za Afrika ya Mashariki VAT siyo juu kiasi hicho. Nchini Kenya ni asilimia 5 na Uganda ni asilimia 18 VAT ni njia nyingine ambayo Watanzania masikini wanalipa kiasi kikubwa cha mapato serikalini kiliko hapo awali. Lakini VAT inafanya vitu viwe ghali zaidi. Kwa hiyo, wakati wanalipa zaidi Serikalini watu wana uwezo wa kununua kidogo zaidi kwa matumizi.

**Wanawake na Wanaume Katika Uchumi wa Tanzania**

Wako wanawake wengi zaidi Tanzania kuliko wanaume, lakini ni robo tu ya watu wanaofanya kazi ya ujira au mshahara ni wanawake. Kwa upande mwingine, zaidi ya nusu ya watu wote wanaofanya kazi katika kilimo ni wanawake. Wengi wa wanawake hao wanaofanya kazi ya kilimo wanalima chakula kwa ajili ya familia zao lakini hawalipwi mishahara.

Wakati wanawake wanapofanya kazi za kulipwa mara nyingi

wanalipwa kidogo kuliko wanaume.Wanawake wanafanya kazi za kulipwa katika kilimo na viwanda wanalipwa chini ya theluthi moja ya kile wanaume wanachopata. Kwa sababu wanawake wachache kuliko wanaume, wanafanya kazi za kulipwa na kwa kuwa wanalipwa kidogo zaidi, wanaume wanachangia zaidi katika mapato ya serikali kuliko wanawake. Lakini wanawake wanachangia kwa njia nyingi zaidi katika jamii.

Wanawake wanawajibika kwa kazi nyingi ambazo hazilipwi hapa nchini. Mbali na kazi zao za kilimo, wanawake wanahusika na kuzaa watoto na kuwatunza wanafamilia wengine. Kama tukijumlisha wanaolipwa mishahara na wasiolipwa wanawake wanatumia saa nyingi zaidi kila siku wakifanya kazi kuliko wanaume. Wanawake hawalipwi chochote kwa kazi nyingi wanazofanya majumbani kwao na wala kwenye jamii zao.

Kazi hizi zisizolipwa za wanawake ni kama kodi. Kodi ni fedha unazolipa kwa jamii ili ifanye kazi kwa ufanisi zaidi. Wanawake na wanaume wanaopata fedha wanalipa kodi ya mapato ambayo serikali hutumia kuhudumia jamii ili iwe inafanya kazi vizuri zaidi .Wanawake wanofanya kazi zisizolipwa, wanaifanya jamii iwe bora zaidi kwa kuwazaa watu na kuwaweka sawa.

Serikali inaweza kuifanya kodi ya kazi isiyolipwa iwe nyepesi zaidi. Inaweza kuwasaidia wanawake katika kazi zao zisizolipwa kwa kuleta maji karibu zaidi na makazi yao, vituo vya afya ambavyo vinaweza kutoa msaada kwa wanawake wajawazito na huduma bure za afya kwa watoto wachanga na watoto wadogo.


**Ni Nani Anayetayarisha Bajeti ya Serikali?**

Kama binadamu, wakati serikali haina fedha za kutosha kwa kila kitu inachotaka kutumia ni lazima ifanye uchaguzi. Ni lazima iamue ni mambo yapi yaliyo muhimu na kuanza kuyashughulikia kwanza. Mambo ambayo serikali inachagua kuwa ni muhimu sana yanaitwa vipaumbele vya serikali.

Kila mwaka Tume ya Mipango inatoa miongozo ya Bajeti kwa Wizara zote, idara na mikoa. Miongozo hii huelekeza wizara na mikoa ni kiasi gani cha fedha watapata mwaka ujao. Miongozo hii pia inaeleza ni vifaa na huduma zipi serikali inafikiria kuwa vipaumbele. Wizara na mikoa wanatayarisha mipango na Bajeti zao kulingana na miongozo hii. Ndipo wanapopeleka mipango na Bajeti zao kwa uamuzi wa mwisho.

Kamati zinazotoa maamuzi ya mwisho kuhusu Bajeti ya nchi ni:

*Kamati ya Mpango na Miongozo ya Bajeti.* Hii inawajumuisha Katibu Mkuu na Makaimu wawili wa Katibu Mkuu wa Hazina, Kaimu Katibu Mkuu wa Tume ya Mipango, Mkurugenzi wa Uwekezaji na Kamishina wa Bajeti.




*Kamati ya Ufundi ya Wizara zote.* Hii ni kamati inayowajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara zote. Huchunguza mipango na kutoa ushauri kwa kabineti.

*Kabineti.* Hii inajumuisha Mawaziri wote. Inajadili ushauri kutoka kwa kamati ya Makatibu Wakuu na kutoa mapendekezo kwa Bunge.

*Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge* hujadili mapendekezo ya Kabineti. Inakaa na viongozi wa wizara zote, mikoa na idara kusikiliza hoja zao kuhusu sababu za kuhitaji fedha walizoomba. Hapo ndipo wanapopeleka mapendekezo yao Bungeni. **Bunge linajumuisha wabunge wote.** Wanajadili mapendekezo ya Kamati ya fedha na Mipango. Baadaye wanayapeleka mapendekezo yao kwa Rais.

Zaidi ya nusu ya Watanzania wote ni wanawake. Lakini idadi ndogo tu ya watu wanatoa maamuzi muhimu kuhusu Bajeti ya serikali ni wanawake. Tume ya Mipango ina wafanyakazi 72. Ni wafanyakazi 11 tu kati ya hao 72 ni wanawake. Nafasi za juu katika Tume ya Mipango ni Katibu Mkuu, Naibu Mkuu na Wakuu 6 wa idara. Hakuna nafasi hata moja kati ya nafasi 8 zinashikwa na wanawake. Hakuna mwanamke yeyote katika nafasi sita za wajumbe wa Kamati ya Mipango na Miongozo ya Bunge. Ni wanawake wawili tu kati ya Wakatibu Wakuu ishirini ambao wanaunda Tume ya Ufundi ya Mawizara. Ni wanawake watatu tu kati ya Mawaziri kamili 23 na wanne kati ya Manaibu




Katibu Mkuu kumi na nne ni wanawake. Ni wanawake watatu tu kati ya wajumbe thelathini wa Kamati ya Fedha Uchumi ya Bungeni.

Ni wanawake arobaini na tano tu kati ya Wabunge 275 wakiwepo wanawake wachache. Hivyo katika utoaji wa maamuzi muhimu, si ajabu kama Bajeti ya serikali haitaweza kukidhi haja za mahitaji ya wanawake.


## Hitimisho

Katika sura hii tumeona kuwa:



**Wanaume wengi zaidi kuliko wanawake wanafanya kazi za kulipwa ujira na mishahara serikalini na biashara binafsi. Wanawake wanapofanya kazi wanalipwa kidogo zaidi kuliko wanaume. Kutokana na hoja hizi mbili, wanaume wanalipa kodi ya mapato zaidi kuliko wanawake. Wanawake wanachangia katika jamii kwa njia nyingine kama vile kuzaa watoto na kutunza familia. Hawalipwi kwa kufanya kazi hizi. Kuwasaidia kufanya kazi hizi vizuri na kuwatunza kwa kazi zisizolipwa, wanawake wanahitaji huduma za serikali kama wanavyopata wanaume. Mara nyingi wanahitaji huduma zaidi kuliko hata wanaume na ni masikini mno kuzilipa.**

**Tanzania ni nchi masikini. Inahitahidi kupata mapato ya kutosha ili kutoa huduma kwa wananchi wote. Kuziba pengo kati ya mapato na matumizi, serikali haina budi kukopa fedha kutoka katika taasisi za fedha kama vile Mfuko wa Kimataifa wa Fedha na Benki ya Dunia. Taasisi hizi zililambia serikali kufanya mabadiliko ambayo tayari yamefanya maisha yawe magumu zaidi kwa watu masikini kupata huduma za afya na elimu.**



### Watu Tofauti wana Mahitaji Tofauti ya Afya


Wanawake na Wanaume wana mahitaji tofauti ya afya. Kwanza, yako mambo kama vile mimba na kuzaa ambayo yanawaathiri wanawake tu. Pili, wanawake wana hatari zaidi ya baadhi ya matatizo ya afya kwa sababu ya mambo wanayoyafanya. Kwa mfano, kazi za wanawake mashambani, kuchota maji na kupata kuni au kazi za nyumbani zinaweza kuwafanya wawe wagonjwa zaidi ya wanaume. Tatu, yako matatizo ya kiafya yanayosababishwa na umasikini wa wanawake wakati wanawake masikini hawawezi kupata chakula kifaacho na cha kutosha na mavazi ya kuwalinda kutokana na maradhi. Nne, wakati wanafamilia ni wagonjwa, ni kawaida wanawake kuwatunza.

Tofauti ya kwanza inatokana na tofauti za kibailojia kati ya wanawake na wanaume - tofauti za kimaumbile. Tofauti ya pili, tatu na nne siyo tofauti za kibailojia. Zinatokana na nafasi walizonazo wanawake katika jamii, na mambo wanayofanya.

Serikali inatambua mahitaji ya afya ya uzazi wa wanawake kuwa ni muhimu sana. Inayaona kama ni kipaumbele cha afya. Kwa mfano, Serikali inasema kuwa hospitali zisiwatoze wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kwa huduma za hospitali. Hata hivyo, serikali haiangalii kwa makini tofauti zisizo za kibailojia za mahitaji ya afya kwa wanawake na wanaume. Hii si haki kwa wanawake. Kama serikali ingejali zaidi mahitaji ya lishe na afya kwa wanawake, itaweza kuongeza hali ya afya kwa vizazi vijavyo. Watu wenye afya wataweza kufanya kazi kwa bidii na kwa ubora zaidi. Wataweza kusaidia kujenga uchumi na jamii ya Tanzania.

Mahitaji ya Afya yanatofautiana kwa umri na pia jinsia. Mtoto wa kike au wa kiume ana mahitaji tofauti na mwanaume au mwanamke wa umri wa kati au mzee.

Chakula ni mojawapo ya mambo muhimu mno kwa afya




nzuri ya watoto wachanga na watoto wadogo. Mtoto ambaye hapati chakula cha kutosha ataathirika maisha yake yote. Serikali inawahudumia watoto wachanga na watoto wadogo kupitia Programu ya Mipango ya Familia, Afya ya watoto na mama. Ni wanawake wanaokwenda kliniki na kutoa matunzo kwa wasichana na wavulana wa umri mdogo.

Katika miaka ya ujana, wasichana na wavulana wanaanza kuwa wanawake na wanaume. Mabadiliko haya yanaleta mahitaji mapya ya afya. Wanawake vijana wana hatari ya kupata mimba. Wakati mama ni kijana, mimba ina hatari zaidi kwa mtoto na mama. Wanawake na wanaume vijana wana hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa kama vile UKIMWI. Wanawake vijana ambao hawajiamini wako katika hatari zaidi kuliko wengine. Vijana wengi zaidi na hususan wavulana wa mjini wameanza kutumia kileo katika umri mdogo. Kitengo cha Afya cha uzazi kina programu ndogo ya elimu kuhusu magonjwa ya zinaa na mimba kwa wanawake vijana.



*Kuzaa kwa kizazi kijacho na uwezo wa mtu binafsi kwa taifa ni dhima ya kibiolojia ya Wanawake. Ni uzingatiaji gani wa Bajeti uliopo kwa Wanawake kwa Wanawake hawa kulingana na hatari inayofuatia?*

Wanawake wanaweza kuzaa watoto wakiwa na umri wa miaka 15 hadi 50. Hii inafahamika kama miaka ya uzazi. Wanawake wa umri huu wanapata hatari nyingi za kiafya. Hatari hizi ni pamoja na mimba zisizo na mpango, utoaji mimba, matatizo wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua na matatizo wanapokuwa na watoto wengi. Watoto wachanga na kinamama wanaofariki dunia wakati wa kujifungua wanafanya takribani robo ya vifo vyote Tanzania. Karibu vizazi 2 kwa kila 1000 hapa Tanzania vinaacha wanawake wamekufa. Wizara ya Afya ina kitengo cha Afya cha uzazi ambacho kinawajibika kwa aina hii ya tatizo. Zaidi ya asilimia 80 ya fedha zote zinazopokelewa kutoka kwa wahisani kutoka nje zinakwenda kwa Afya ya Mama na Mtoto.

Wanawake wanaishi maisha marefu zaidi kuliko wanaume kwa hivyo wako wanawake wazee zaidi kuliko wanaume Tanzania. Wanawake wazee wana matatizo mapya ya afya. Baadhi ya matatizo hayo yanatokana na "menopozi". Matatizo mengine yanatokana na udhaifu wa umri mkubwa. Udhaifu huu unafanya wanawake wawe na matatizo ya kufanya kazi kama hapo awali . pia kujihudumia. Matatizo mengine yanatokana na umasikini wakati wanawake hawawezi kulipia mahitaji yao mapya. Umasikini ni mbaya zaidi wakati familia zinapowatelekeza

wajane na wanawake wengine wazee. Serikali haijali sana mahitaji ya afya ya wanawake wazee.


**Sera ya Afya Tanzania**

Baada ya uhuru, serikali ya Tanzania ilidhamiria kutoa huduma za afya kwa wananchi wake wote. Katika adhima hii, mwaka 1977 serikali ilipiga marufuku hospitali binafsi. Ilisema kuwa madaktari na hospitali zisipate faida kutokana na afya. Badala yake, wananchi wote wanapaswa kupata bure huduma za afya. Leo, karibu robotatu ya Watanzania wote wana kituo cha afya chini ya kilomita tano kutoka pale wanakoishi. Asilimia tisini wana kituo cha afya chini ya kilomita 10 kutoka wanakoishi.
Azimio la Arusha lilisema kuwa ni lazima kuwe na huduma za afya kwa ajili ya watu waishio vijijini. Huduma za afya zisiweko tu mjini. Hii ni muhimu kwa wanawake masikini, wengi wao wanaoishi vijijini.

Mwaka 1983 serikali iliamua kuwa huduma za msingi za Afya lazima ziwe ni kitovu cha sera ya afya. Huduma za msingi zinasema kuwa tusisubiri hadi mtu anapokuwa mgonjwa na baadaye tujaribu kumfanya awe na afya tena. Badala yake tunapaswa kujaribu kuzuia watu wasiugue. Huduma za msingi za afya zinasema kuwa maji safi, vyoo vizuri na lishe bora ni muhimu kwa afya kama walivyo madaktari na manesi. Huduma za msingi za afya zinasema kuwa chanjo na programu za afya kwa wanawake na watoto ni muhimu zaidi kuliko operesheni tata zilizo ghali katika hospitali.

Mwaka 1990 serikali ilibadilisha sera ya afya ili kutoa umuhimu zaidi kwa wilaya nchini. Ilijaribu pia kutafuta njia nyingine kama vile mashirika ya hiyari, huduma binafsi na michango ya jumuiya kuongezea juhudi za serikali katika afya. Ilisema kuwa hii ilikuwa ni lazima kwa sababu Bajeti ya serikali haikuwa kubwa ya kutosha kutoa huduma kwa kila mtu.

Mwaka 1996 zilikuwepo hospitali 4,910, huduma za afya na




zahanati Tanzania. Zaidi ya nusu (2,642,) zilimilikiwa na serikali na 1,290 zilikuwa za watu binafsi ambapo 774 zilikuwa za mashirika ya hiari kama vile mashirika yasiyo ya serikali na makanisa na 204 ziliendeshwa na mashirika ya umma. Hii ina maana kuwa serikali ilioanza kushindwa kuhudumia wananchi wake kiafya, kama ilivyokuwa inatarajia. Leo hii huduma za afya mara nyingi hazitolewi bure. Wanawake na wanaume wanaotumia huduma binafsi inawabidi wazilipie kwa ajili ya afya zao. Ni lazima walipe wakati wanapotumia hospitali za serikali pia. Na serikali inataka kuanza kutoza kwa huduma za vituo vya afya na zahanati.

Serikali inasema kuwa huduma za afya kwa kinamama wajawazito ni lazima ziwe bure. Lakini kinamama wengi wanalazimika kulipa wanapokwenda hospitali za serikali kujifungua. Ni lazima wachukue glovu kwa manesi na daktari, padi na vifaa vingine.

### Wahisani wa Nje na Mipango ya Uwekezaji wa Kisekta

Wako wahisani wengi wa nje wanaotoa fedha kwa huduma za afya Tanzania. Wahisani wa nje wanatoa zaidi ya asilimia 90 ya

bajeti ya maendeleo ya afya. Siku za nyuma wahisani hawakujadiliana miongoni mwao juu ya kile wanachotaka kufanya. Hivyo baadhi ya mikoa na wilaya zingine hazikupata misaada hiyo ya wahisani.

Mwaka 1997 serikali iliamua kuwa na mpango wa uwekezaji wa sekta. Mpango huu unaeleza mahitaji muhimu ya afya yalivyo hapa nchini. Serikali inasema kuwa wahisani wa nje wanapaswa kutoa fedha kulingana na mpango huu.

Watu wengi wanasema kuwa mpango huu wa uwekezaji wa sekta hautatatua matatizo yaliyopo. Wanasema kuwa mpango huu unajumuisha mambo mengi mno. Wanasema hata kwa misaada ya wahisani, serikali haitaweza kukidhi mahitaji yote kwa kipindi cha miaka michache ijayo. Wanasema serikali haina budi kutayarisha mpango mfupi zaidi. Mpango unapaswa kusema kwa uwazi zaidi ni mahitaji yapi muhimu yaliyopo.Vinginevyo iko hatari kwamba mahitaji yasiyo muhimu yatashughulikiwa kabla ya yale yaliyo muhimu.

Tatizo jingine ni kuwa wahisani hawaiambii serikali kwa uwazi kiasi gani wanachotoa. Wakati mwingine wanazungumza na wananchi vijijini na kutoa fedha na misaada mingine moja kwa moja. Haya yanapotokea, ni vigumu kwa serikali kuona kuwa fedha na misaada mingine inatumika kwa usawa kati ya sehemu mbalimbali za nchi.

**Bajeti ya Afya**

Wizara ya Afya imegawanywa katika idara mbalimbali:

- **Hospitali na Huduma za Tiba** husimamia hospitali zinazo jitahidi kuwafanya wawe na afya wanapougua.
- **Huduma za Kinga na Mazingira** inajitahidi kuzuia maradhi. Inajaribu kudhibiti magonjwa kuwafanya wanawake na watoto wawe na afya na kuhakikisha kuwa watu wanaishi katika hali nzuri kwa ajili ya afya zao.
- **Mkemia Mkuu wa Serikali** anahakikisha kuwa dawa za aina


zote ni za kiwango cha juu.

- **Ghala ya Dawa** inanunua dawa na vifaa na kuvisambaza kwenye hospitali na wilaya.

Bajeti ya Wizara ya Afya siyo Bajeti pekee ambayo serikali inatoa fedha kwa ajili ya afya. Hadi mwaka 1997/98 kulikuwepo na fedha kwa ajili ya afya katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Bajeti hii ilikuwa na fedha kwa kila mkoa. Kila mkoa uligawa fedha hizi kwa wilaya zake. Kuanzia mwaka1998/99 fedha kwa ajili ya mikoa hazitatoka katika Bajeti ya Wizara bali katika wizara mpya ya serikali za Mitaa.

Mwaka 1977/78 mara baada ya Tanzania kuwa huru, asilimia 7.5 ya matumizi ya serikali yalikwenda afya. Miaka kumi baaadaye serikali ilitoa fedha kidogo kwa afya kila mwaka. Mwaka 1987/88 ni asilimia 3.9 tu ya matumizi ya serikali yalikwenda afya. Tangu wakati huo mgao umekuwa mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1977/78. Mwaka 1996/97 asilimia 12.3 ya matumizi ya serikali yalikwenda afya. Mwaka 1996/97 Bajeti ya serikali kwa ajili ya afya ilikuwa Tsh. 47,589m/=. Wataalamu wengi wa afya wanasema kuwa hii bado haitoshi kukidhi mahitaji ya afya Tanzania.

**Bajeti ya Serikali ya Afya 1994/95**



*Jedwali 3.1* **Bajeti ya Serikali kwa ajili ya Afya 1994/95 (Tsh m/=)**

| Aina | Kawaida | Maendeleo | Mhiasni | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Tiba | 51,027 | 1.127 | 2,539 | 54,693 |
| Kinga | 3,840 | 376 | 5,843 | 10,059 |
| Utawala | 285 | 15 | 0 | 300 |
| Mafunzo | 1,787 | 1,610 | 0 | 1,870 |
| Mengine | 28 | 9 | 0 | 37 |
| Jumla | 56,968 | 1,610 | 8,382 | 66,960 |

Jedwali 3.1 linaonyesha kuwa matumizi makubwa ya Serikali kwa afya yalikuwa ni kwa ajili ya huduma za tiba. Mwaka 1994/95 asilimia 90 ya matumizi ya kawaida na asilimia 70 ya matumizi ya Serikali kwa maendeleo yalikuwa kwa ajili ya huduma za tiba. Matumizi ya Serikali hayaendani na sera ya Serikali ya afya. Sera ya afya inasema kuwa huduma ya msingi ya afya na kinga ni mihimu zaidi kuliko tiba.

Wahisani walitoa zaidi kwa huduma za kinga. Na wakati wahisani walipotoa kwa huduma za tiba, walitoa zaidi zahanati na vituo vya afya kuliko hospitali kuu.

Zahanati na vituo vya afya vinaleta huduma za afya karibu zaidi na wanawake na wanaume masikini wanaohitaji zaidi huduma hizi.


Bajeti nyingi za kawaida za serikali hutumika kulipia ujira na mishahara. Hii inaacha kiasi kidogo sana kwa ajili uendeshaji wa gharama nyingine. Katika vituo vya afya na zahanati, theluthi mbili ya Bajeti huenda kwenye mishahara na robo moja kwa dawa. Hii inabakisha asilimia 7 tu kwa matumizi mengine. Katika hospitali kubwa, chini ya robo ya Bajeti inatumika kwa mishahara asilimia 7 kwa dawa na asilimia 70 zinabaki kwa gharama nyingine.


Shilingi tatu kwa kila shilingi mia zinazotumika hospitali hulipia watu wanaokwenda ng'ambo kwa ajili ya huduma ya afya. Mara nyingi ni viongozi wa juu na familia zao wanaokwenda ng'ambo kwa huduma ya afya . Maofisa hawa wana fedha zaidi kuliko Watanzania walio wengi. Fedha zinazotumika na serikali kuwapeleka watu wachache ng'ambo zingeweza kutumika vizuri zaidi. Zingeweza kugharamia mpango wa familia na huduma wakati wa ujauzito na kujifungua kwa maelfu ya wanawake na vijijini.

## Hali ya Wafanyakazi (Wanawake na Wanaume) wa Sekta ya Afya

Wafanyakazi wengi wa sekta ya afya ni wanawake. Hususan manesi wengi ni wanawake. Wafanyakazi wa afya walioajiriwa na serikali wanafaidika na bajeti ya serikali wanapopata mishahara yao. Hata hivyo, kwa jumla wanawake walioajiriwa na serikali hufaidika kidogo zaidi kuliko wanaume wenzao. Hii ni kwa sababu wengi wa walio na vyeo vya juu ni wanaume. Watu hawa na wengine wa ngazi za juu wanapata mishahara mikubwa zaidi. Wanafanya maamuzi muhimu yanayowaathiri wanawake pia.

**Wafanyakazi Wanawake na Wanaume katika Sekta ya Afya 1995**







Mwaka 1995 ni asilimia 11 ya mabingwa , asilimia 15 ya madaktari wa kawaida na asilimia 8 ya madaktari wa meno na asilimia 7 ya mafamasia ni wanawake. Kwa upande mwingine asilimia 99 ya wasaidizi wa uzazi na afya ya watoto, asilimia 87 ya manesi wa kawaida, asilimia 79 ya wahudumu wa hospitali walikuwa wanawake. Madaktari wa kawaida na wa meno wanapata mishahara mikubwa na wana uwezo kuliko wahudumu wa afya, manesi, wasaidizi wengine.

Wanawake na wanaume wanaofanya kazi hospitalini, katika zahanati na vituo vya afya wanalipwa kwa kazi hii. Watu wengine wengi hutoa huduma za afya bure wanapowatunza wanafamilia ambao ni wagonjwa. Mara nyingi ni wanawake wanaotoa huduma hii bure.

Serikali inategemea kazi hii isiyolipwa wakati wanafamilia wako hospitalini. Kwa mfano, Hospitali ya Muhimbili inatoa chakula tu kwa wagonjwa katika wodi za daraja la kwanza na pia wagonjwa wanaoletwa kutoka mikoani. Wagonjwa wengine wanapaswa kutegemea wanafamilia hususan wanawake kwa kuwaletea wagonjwa chakula.

## Wasichana na Wanawake na Bajeti ya Serikali ya Afya

Mapema tumeona kuwa wanawake wana mahitaji tofauti wakati tofauti wa maisha yao. Hapa tunaona fedha zinazolipwa na



MPs pass Bill to provide health insurance funds to civil servants

serikali kukidhi mahitaji haya.

***Watoto na Wazazi***

Mfumo wa huduma za msingi za afya ni muhimu sana kwa afya ya wasichana na wavulana wadogo na kwa afya za mama zao. Serikali ya Denmark ilitoa US$ 9.3 Millioni kwa Tanzania kwa huduma za msingi wa afya kati mwaka 1989 na 1996. Serikali za Denmark, Marekani na Japan, Shirika la Afya Duniani, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Elimu kwa Watoto, klabu ya Kimataifa ya Rotary kwa pamoja wametoa US$7,125 Millioni kwa kukinga maradhi kwa kipindi hicho. Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Elimu ya Watoto na Serikali ya Japan zilitoa fedha kwa afya ya kina mama na mtoto katika wilaya. Serikali ya Tanzania ilitoa US$ elfu 16 kati ya mwaka 1989 na 1996 kwa miradi ya afya kina mama na watoto.

Kwa msaada wa wahisani, fedha nyingi zinakwenda kwa afya ya kina mama na watoto. Lakini Tanzania inafanikiwa kidogo kuliko Kenya ambayo inapata kiasi kidogo zaidi. Tafiti mbali mbali zinaonyesha kuwa, Wakenya wanaishi miaka minane zaidi kuliko Watanzania. Ni theluthi moja tu ya watoto wanaokufa Kenya kulinganishwa na Watanzania. Na mwanamke wa Kenya kwa wastani ana watoto mmoja pungufu ya mwanamke wa Tanzania. Kwa familia masikini watoto wachache inamaanisha afya bora zaidi kwa sababu hawawezi kumudu kupata chakula kwa wote.

***Vijana***

Kuna kiasi kidogo cha fedha katika bajeti ya taifa kwa ajili ya

kuwaelimisha vijana kuhusu mabadiliko ya miili yao. Kitengo cha afya ya uzazi kina mipango michache ya elimu kwa vijana juu ya magonjwa ya zinaa na mimba za mapema. Kwa mfano, Serikali ya Marekani inasaidia mradi wa mpango wa familia. Mwaka 1998/99 walitoa Tsh. 588m/= kwa ajili ya mafunzo, Tsh54m/= kwa ukunga katika jumuiya, Tsh. 80m/= kwa ajili ya kwenda mikoani, Tsh. 181m/= Mipango, Tsh 195m/= kwa habari na Tsh188m/= kwa utawala. Ni kiasi kidogo tu cha fedha hizo kitakachokwenda kwa vijana.

***Wanawake wa Umri wa Kuzaa***

Mwaka 1993 asilimia 80 ya hospitali zote, vituo vya afya na zahanati zilitoa huduma za mama na mtoto, na asilimia 69 zilikuwa na mpango wa familia na uzazi bora.



Vifaa vingi vya mama na mtoto vilitengenezwa kwa kutumia fedha kutoka serikali ya Marekani. Serikali ya Marekani ilisitisha kutoa fedha hizi kwa muda na baadhi ya huduma hazikufanya kazi vizuri. Mradi wa Mpango wa Familia utasaidia kuwezesha kufanya kazi vizuri tena .

*"Ndiyo tunahitaji bajeti ya maendeleo na mgao wa rasilimali za Taifa ambao haubagui. Wasichana na wavulana tushirikishwe katika mchakato wa Bajeti."*

Huku kuanza na kusita kwa miradi muhimu ya afya ni sehemu ya hatari ya kutegemea fedha kutoka nje. Kama serikali ingetoa fedha zaidi kwa afya ya mama na mtoto, kutakuwepo na hatari kidogo ya huduma ya afya kwa kwenda juu na chini.



*'Usalama wa mama utawezekana tu kama Bajeti na mchakato wa mgao wa rasilimali ya taifa unachukulia kwa makini kwa vipengele hivi muhimu na kuwekeza katika njia hii muhimu.'*

Kwa ajili ya afya nzuri ya mtoto wake na yeye pia mwanamke mjamzito anapaswa kupata huduma za afya walau mara sita wakati wa ujauzito wake. Wakati wa kwenda kupata huduma hizi, damu na mkojo vitachunguzwa. Wanawake wengi hawaendi kupata huduma hizi kama ilivyoelezwa hapo juu. Baada ya kujifungua, mama anapaswa kupumzika hospitalini au kituo cha afya takribani kwa saa 24. Wanawake wengi nchini huondoka baada ya saa 6 tu.

Wanawake wenye uwezo kiuchumi, wanaoweza kulipa malipo ya juu hupata huduma bora zaidi wanapokuwa wajawazito. Wanawake wengi wa Tanzania hawawezi kumudu kutumia fedha nyingi kwa afya zao. Uzazi ni gharama hata kwa wanawake wanaotumia hospitali za serikali. Kwa mfano, wanawake wanaopata watoto wao katika hospitali ya Muhimbili wanapaswa kuleta pea mbili za glovu, maboksi mawili ya padi, kemikali ya kuua viini vya maradhi, sirinji mbili, dawa, mashuka manne na shuka kwa ajili ya mtoto.

Hivyo hata kama wanawake hawalipi ada ya hospitali, wanalipa kwa njia nyingine wakati wa uzazi.

***Wanawake Wazee***

Wanawake wengi wazee wanateseka kwa maradhi ya moyo, mifupa na kisukari. Wana matatizo pia ya ovari, tumbo la uzazi na matiti. Huduma muhimu sana kwa wanawake wazee ni kuchunguzwa mara kwa mara ili matatizo yao kiafya yaonekane mapema. Huduma za afya za serikali ya Tanzania hazitoi uchunguzi huu. Hata hivyo, kuna taarifa kidogo sana kuhusu matatizo ya wanawake wazee Tanzania. Kwa mfano, mwaka 1995/96, Bajeti ya serikali haikutoa fedha zozote kwa utafiti juu ya mada hii au mada nyingine.

**Umma au Binafsi?**

Mwaka 1993/94 takribani asilimia 58 ya wagonjwa wote walikwenda kupata huduma ya afya serikalini kwa tiba ya kwanza.

Kati ya idadi ya watu wote waliopata huduma za serikali, wengi wa walio masikini sana walikwenda zahanati au kituo cha afya. Watu walio tajiri walikwenda zaidi katika hospitali za kati. Inagharimu serikali fedha nyingi kumtibu mtu katika hospitali ya kati kuliko kumtibu katika zahanati au kituo cha afya. Katika ulinganisho huu kwa jumla, serikali ilitumia fedha zake zaidi kwa afya ya watu tajiri kuliko inavyotumia kwa afya ya watu masikini.

**Kutumia Zaidi Serikali Inahitaji Mapato Zaidi**

Serikali inataka kutumia fedha zaidi kwa ajili ya afya lakini inasema haina kiasi hicho cha fedha. Ili kutatua tatizo inajitahidi kutafuta njia mpya za kuongeza mapato. Njia mojawapo mpya ni kwa kutoza ada. Kwa sasa ni katika hospitali tu ndiko watu hulipa ada. Mwaka 1995/96 hospitali ya Muhimbili ilikusanya Tsh. 89m/= kama ada kutoka kwa wagonjwa. Hospitali za Rufaa na za mikoa zilikusanya takribani Tsh. 249m/=. Kiasi hiki ni pungufu kuliko kile kilichokusanywa mwaka 1994/95.

Serikali sasa inataka watu waanze kulipia huduma za tiba katika vituo vya afya na zahanati. Wanajaribio la shughuli hii ya ada katika wilaya chache. Lakini wanajua kuwa watu wengi hawatalipa kwa huduma za afya wilayani hadi hapo ubora wa huduma utakapokuwa mzuri.

Utafiti unaonyesha kuwa Watanzania wengi hawaridhiki na huduma za afya serikalini. Takribani theluthi mbili wanasema kuwa hakuna dawa za kutosha, asilimia 45 wanasema kuwa huduma ziko mbali mno na asilimia 25 wanasema kuwa wafanyakazi hawana sifa za kutosha. Watu wengi walisema kuwa watalipa huduma hizo kama ubora wake utakuwa mzuri.


Huduma nyingine zinaigharimu serikali fedha zaidi kuliko nyingine. Huduma nyingine zinaleta mabadiliko makubwa kwa afya za wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wa Tanzania kuliko nyingine.

Huduma nyingine zinaokoa fedha kwa sababu afya mbaya inazuiwa na hivyo serikali na mgonjwa hawalipi fedha zaidi baadaye. Wakati huduma inapoleta mabadiliko kwa kiasi kidogo cha fedha au inapozuia matumizi makubwa baadaye, tunasema kuwa huduma hiyo gharama itakiwayo.

Baadhi ya huduma za afya zenye gharama zitakiwazo ni:


- Kuzuia mimba zisizotakiwa,
- Kuzuia maradhi ya zinaa,
- Mimba na uzazi salama,
- Huduma bora kwa wanawake wajawazito,
- Msaada wa chakula kwa watu walio katika nafasi dhaifu,
- Uchunguzi wa sarakani ya ziwa na sarakani ya mlango wa kizazi.

# Tunataka Mabadiliko Yapi katika Bajeti ya Afya ya Serikali?




Tunataka fedha zaidi ziwaelimishe wanawake vijana kuhusu mabadiliko ya mili yao. Tunataka matumizi mazuri zaidi ya fedha kwa afya ya wazazi na watoto. Tunataka huduma zaidi kwa mahitaji ya wanawake wazee. Wanawake wasionekane kama hawafai wakati wanaposhindwa kuzaa watoto.

Tunataka kufahamu zaidi juu ya namna serikali inavyotoa huduma kwa mahitaji ya wanawake na wanaume. Tunataka serikali itoe ripoti ya idadi ya wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanaopata huduma. Tunataka watoe ripoti ya aina mbalimbali za huduma wanazopata wanawake, wanaume, wasichana na wavulana.



Tunaitaka serikali kutoa fedha zaidi kwa huduma zenye gharama zitakiwazo na fedha kidogo kwa matibabu ghali kwa watu wachache. Hatutaki fedha zisipotezwe nchi za nje kuwatibu watu wanaoweza kujilipia.



## Utangulizi

Kabla ya mwaka 1990 Wizara za Elimu na Utamaduni na Serikali za Mitaa zilikuwa na wajibu wa elimu yote nchini Tanzania. Mwaka 1990 serikali iliunda wizara mpya, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Leo hii Wizara za Elimu na Utamaduni na Serikali za Mitaa zinawajibika kwa elimu ya msingi na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu inawajibika kwa elimu ya juu. Hadi mwaka 1998 serikali za Mitaa zilipata Bajeti zao kutoka katika ofisi ya Waziri Mkuu. Leo kuna wizara mpya ya Serikali za Mtaa inayotoa fedha mikoani na wilayani kwa ajili ya elimu, afya, maji na mambo mengine.



*Wasichana hawa wadogo, ndoto zao za muda mrefu ni kushika nafasi za juu katika vyombo vya serikali vinavyotoa maamuzi. Fikra za Bajeti ya Jinsia zinahitajika kuwatayarisha ili ndoto yao iwe ya ukweli.*

Sura hii inaangalia Bajeti za Wizara mbili zinazobeba Elimu ya nchi. Inaangalia pia kile kinachotokea katika elimu hasa wilayani.

## Historia ya Elimu Tangu Uhuru

Wakati Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961 walikuwepo wasichana wachache kuliko wavulana katika shule za sekondari na wanawake wachache katika Chuo Kikuu. Nchi iliamua kuongeza idadi ya wavulana na wasichana katika ngazi zote za elimu ili kuwapata wanawake na wavulana wasomi kuweza kufanya kazi serikalini. Katika kutekeleza uamuzi, mwaka 1965 serikali iliacha kudai ada kwa shule za sekondari ili wavulana na wasichana wapate elimu katika ngazi hii.

Serikali ilikuwa na nia ya kuimarisha elimu ya watu wazima kama ilivyo kwa vijana. Ilitangaza mwaka 1970 kuwa mwaka wa Elimu ya Watu Wazima. Kulikuwepo kampeni kubwa mjini na vijijini kuwahimiza watu wazima wajifunze kusoma na kuandika.

Kampeni ilikuwa ya mafanikio makubwa, hasa katika kugusa mahitaji ya elimu ya wanawake na wanaume masikini.

Mwaka 1971 serikali ilichukuwa shule zote binafsi na mamlaka kwa mikoa na wilaya kusimamia elimu ya msingi. Mwaka 1972 serikali ilitayarisha sera mpya kwa ajili ya shule za sekondari. Ilisema kuwa wanafunzi na walimu wa kila shule lazima wasaidie kujikimu kwa kuzalisha moja ya tano ya chakula chao. Mwaka 1974 lazima kuwe na shule za kutosha kutoa elimu kwa watoto wote nchini. Sera hiyo ilisema pia kuwa elimu lazima iwe ya bei nafuu - shilingi ishirini tu kwa mwaka mzima.




*Kuwekeza katika elimu kunaonyesha utambuzi wa serikali kwa watu wake, wasichana na wavulana.*

Sera zote hizi zilikuwa na mafanikio na walikuwepo wanafunzi wengi zaidi shuleni Tanzania. Hata hivyo, kuwepo kwa wanafunzi wengi bila ya rasilimali ya taifa kuongezeka kwa kasi katika sekta ya elimu kulileta matatizo. Kwa mfano, hawakuwepo walimu waliosomeshwa wa kutosha na pia vitabu havikuwa vya kutosha. Wahisani wa nje walisaidia kutoa vitabu lakini hawakutaka kusaidia gharama zinazoendelea kama vile mishahara ya walimu. Hivyo ubora wa elimu ulianza kuwa sio mzuri.

Wakati wa kipindi cha miaka ya 1980 matatizo ya kushuka kwa elimu yalikuwa makubwa zaidi. Kukiwa na uchumi dhaifu serikali ilikazia zaidi katika sera ya uchumi kuliko sera za afya na elimu. Mwaka 1993 serikali ilisema kuwa wazazi wanapaswa kuchangia gharama za elimu na serikali. Leo wazazi wanapaswa kulipa mchango wa UPE wa Tsh. 1,000/= kwa sare ya shule, Tsh 200/= kwa usalama na Tsh. 2,100/= kwa vitabu. Wazazi wa watoto wa shule za sekondari lazima walipe ada ya shule, ada ya mitihani pamoja na fedha za vitabu, vifaa vya kuandikia na usafiri. Kiasi kinacholipwa na wazazi kimepanda juu zaidi kuliko kile kinacholipwa na serikali.

Leo wazazi wengi hasa wa vijijini hawawezi kumudu kuwapeleka watoto wao shuleni. Mwanzoni mwa miaka 1980 kulikuwepo na wanafunzi mara 10 zaidi kuliko miaka 20 iliyopita. Katikati ya miaka ya 1980 kulikuwepo wanafunzi mara 10 zaidi ya asilimia 90 ya watoto wenye umri wa kwenda shule walikuwa shuleni. Lakini baada ya kupungua kwa fedha za serikali kwa ajili ya elimu, mwaka 1995 chini ya asilimia 80 ya watoto tu wenye umri wa kwenda shule walikuwa shuleni.

**Nafasi za Wanafunzi wa Shule za Msingi Waliojiunga na Sekondari 1997/98**




Leo mtoto wa Kitanzania ana nafasi finyu kuliko mtoto wa nchi nyingine za Afrika Mashariki ya kwenda shule ya sekondari. Ni asilimia 5 tu ya wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania wanaendelea na masomo ya sekondari. Nchini Uganda ni asilimia 11 wanaoendelea na Kenya ni asilimia 25. Kuwepo kwa matatizo shuleni kuna athari kubwa kwa wasichana wa Tanzania yako matatizo mengi kuliko kwa wavulana wa Tanzania. Robo ya wanafunzi wa kike wanaacha masomo wakati wakiwa shule za msingi na asilimia 17 kwa miaka ya kwanza ya sekondari. Mwaka 1995 asilimia 14 ya wasichana walishindwa mitihani yao ya kidato cha nne ikilinganishwa na asilimia 6 ya wavulana. Vilevile, wakati wazazi hawana fedha za kutosha kwa watoto wote wao wa kiume kuliko wale wa kike.

Idadi ndogo ya wasichana katika shule za sekondari inamaanisha wanawake wachache Chuo Kikuu. Idadi ya wanawake kwa kozi za sayansi ni ndogo sana. Baadhi ya vyuo vikuu vimejaribu kurekebisha hali hii. Kwa mfano wametayarisha programu mahsusi. Vimetoa pia fedha kwa mafunzo katika masomo ambayo yana wanawake wachache tu. Lakini hadi hapo wanawake wengi zaidi watakapokuwa shule za sekondari, mawazo haya hayawezi kuleta tofauti kubwa.

**Bajeti ya Elimu**

Elimu, afya na maji kwa pamoja hufanya sekta ya jamii. Kwa kipindi cha miaka michache iliyopita sehemu ya Bajeti inayotolewa kwa sekta za jamii imeshuka. Keki ya serikali kwa huduma za jamii imekuwa ndogo. Hata hivyo elimu imepata sehemu kubwa ya mgao wa keki hii ndogo. Hii inaifikisha Tanzania kuwa nchi yenye bajeti ya elimu ndogo kuliko nchi nyingine za Afrika ya Mashariki.


Friday, June 4, 1999 ECONOMIC INDICATORS BUSINESS TIMES

**Low budget harms education**

Mwaka 1996/97 elimu ilipata asilimia 65 ya Bajeti ya kawaida katika sekta ya jamii na 33 kwa Bajeti ya Maendeleo.

- Zaidi ya nusu ya Bajeti ya Elimu ni kwa ajili elimu ya msingi,
- Robo ni kwa ajili ya elimu ya juu,
- Asilimia 8 ni kwa ajili ya elimu ya sekondari,
- Asilimia 5 ni kwa ajili ya elimu ya ualimu,
- Asilimia 5 ni kwa ajili ya utawala,
- Takribani asilimia 10 ya bajeti za serikali za mitaa zinatumika kwa elimu ya msingi na sekondari.

Elimu inakuwa ghali zaidi kwa serikali na wazazi katika ngazi ya juu. Serikali inatumia mara sita zaidi kwa mwanafunzi wa sekondari kuliko yule wa shule ya msingi. Inatumia mara nane zaidi kwa mwanachuo wa mafunzo ya ualimu kuliko yule wa shule ya msingi. Inatumia zaidi mara mia kwa mwanachuo wa Chuo Kikuu kuliko yule wa shule ya msingi.

Wizara zinazohusika na elimu zinasema kuwa Bajeti zao ni finyu mno. Mwaka 1997/98 Wizara ya Elimu na Utamaduni ilisema kuwa ilihitaji Tsh. 40,273m/= lakini ilipata zaidi ya robo ya kiasi hicho - Tsh. 13,975m/= Wizara ya Sayansi , Teknolojia na Elimu ya Juu ilisema kuwa inahitaji Tsh. 34 b/= kama matumizi ya kawaida lakini ilipata Tsh.23b/=.

**Shule za Msingi**

Mwaka 1997 walikuwepo wanafunzi 3,961,620 katika shule za msingi nchini. Chini ya nusu ya wanafunzi hawa walikuwa wasichana. Lakini kama tulivyoona mapema kuna wasichana na wavulana wachache katika shule kuliko ilivyokuwa miaka 10 iliyopita.


Shule zote za serikali za msingi ziko wazi kwa wavulana na wasichana. Ziko shule chache binafsi zilizo kwa ajili ya wasichana tu.

Watoto wengi wanaoanza shule hawaendi hadi mwisho wa elimu ya msingi. Watoto wengi wana umri zaidi ya miaka 7 wanapoanza shule. Kwa wasichana hii ina maana kwamba watakuwa vijana na wana hatari ya kupata mimba - wakati bado wako shule ya msingi. Hali ya wanaoacha masomo kutokana na mimba ni mbaya sana katika mikoa ya Lindi na Ruvuma mahali ambapo takribani moja ya tano ya wote wanaoacha shule ni kutokana na sababu hii.

Baadhi ya wasichana masikini wanaacha kwenda shule kutokana na kazi wanazofanya nyumbani kama vile kupika, kufagia na kuwatunza wadogo zao.Wavulana masikini wanaacha kwenda shule ili kupata fedha kwa ajili ya familia zao.

Kwa wastani wasichana wanapata asilimia 31 chini ya wavulana kwa mtihani wa mwisho.

Ziko wilaya tatu tu ambazo wasichana wanafanya vizuri zaidi kuliko wavulana katika mitihani ya shule za msingi. Wilaya hizi tatu ziko katika mkoa wa Kilimanjaro. Wasichana katika miji kwa kawaida hufanya vizuri zaidi kuliko wenzao wa vijijini. Hii




inaonyesha kuwa wasichana katika maeneo yenye maji ya bomba na huduma nzuri za afya wanafanya vizuri kuliko wasichana katika maeneo yasiyokuwa na huduma hizi. Pia wasichana wanapovunja ungo hawatapenda kwenda shule kama hakuna vyoo na maji.

Serikali hutumia kwa wastani US$ 23.96 kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na wazazi wanalipa US$ 7.76. Takribani nusu ya sehemu ya Matumizi ya wazazi ni kwa ajili ya sare ya Shule. Hii inabakisha kiasi kidogo sana kwa matumizi mengine muhimu.



*Huu ni mfano halisi wa kutokuwekeza katika elimu na jinsi inavyoathiri watoto wakiwemo watoto wa kike.*

Serikali imekopa US$ 5 milioni kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya mfuko wa Elimu ya Jamii. Serikali inataka kutumia fedha hizi ili kuwapata watoto wengi shuleni. Itatumia kiasi cha fedha hizi kwa ajili ya majengo bora zaidi, vifaa, n.k. kujaribu kuboresha ubora wa elimu. Kwa sasa kuna deski moja kwa watoto watano katika shule za msingi. Hakuna meza za kutosha na viti vya walimu wote. Lakini ipo tofauti kubwa kati ya wilaya. Katika wilaya nyingine wako wanafunzi 400 au zaidi kwa darasa moja.

Kila shule inaweza kupata sh 6,000/= kwa kila mwanafunzi kutoka katika mfuko wa Elimu ya Jamii. Shule zitaweza tu kupata fedha kutoka katika mfuko huo kama wazazi watatoa sh. mbili kwa kila shilingi moja inayotolewa na wazazi. Katika maeneo tajiri mfuko utatoa kiasi kilicho sawa kama wazazi.

**Shule za Sekondari**

Kabla Sera ya Elimu haijabadilika, zaidi ya nafasi za shule za sekondari kwa kila wilaya ilijikita katika idadi ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi. Theluthi moja ilitolewa kwa wasichana.

Wakati idadi ya watoto wa shule za msingi ilipopanda serikali haikuwa na nafasi za kutosha katika shule za sekondari kwa watoto wote wanaomaliza shule ya msingi. Mara nyingi, ilikuwa ni familia tajiri tu ambazo zilimudu karo ya shule binafsi.

Mwaka 1985 serikali iliomba kila mkoa kutayarisha mpango wa miaka kumi. Ilisema kuwa wakati wa miaka hiyo 10 watu katika jamii wanapaswa kuchangia fedha na jasho lao katika kujenga shule mpya za kutwa kwa wasichana na wavulana. Serikali ilisema kuwa shule ni lazima ziwe za kutwa kwa sababu shule za kulala ni ghali zaidi kuendesha. Ilisema kuwa ni lazima kuwe na idadi sawa ya wasichana na wavulana katika shule zote hizi.

Mikoa mingine iliamua kujenga zaidi ya shule nne. Wizara ya Elimu haikuwa na walimu wa kutosha na vifaa vingine kwa shule zote mpya ili ziendeshwe vizuri.

Serikali imejitahidi kuongeza idadi ya wasichana katika shule za sekondari. Imeongeza madarasa ya kutoa katika shule za kulala. Imetengeneza malazi kwa wasichana katika shule za wavulana. Imeshikilia sheria isemayo kuwa theluthi ya nafasi lazima iende kwa wasichana.

Wasichana wengi zaidi kuliko wavulana wanaacha shule. Ni robo tu ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha 5 ni wasichana. Hii ni mara mbili bora zaidi kuliko miaka ya 1960 wakati moja ya nane ya wanafunzi wa shule ya juu ya sekondari walikuwa wanawake. Lakini bado siyo nzuri ya kutosha.

Wanafunzi katika shule za wavulana tu wanafanya vizuri sana mitihani yao. Mwaka 1995 ni asilimia 8 tu walioshindwa mitihani yao. Wanafunzi katika shule za wasichana wanapata alama za chini kidogo. Mwaka 1995 asilimia 21 walishindwa. Wanafunzi katika shule za mchanganyiko walipata alama za chini sana. Zaidi ya robo walishindwa mitihani yao.

Wasichana wanaoacha masomo au wanashindwa kutokana na sababu zinazofanana katika shule za sekondari na shule za msingi. Baadhi yao wanaolewa au wanazaa mapema. Wengi wao

wana shughuli nyingi za kufanya wakiwa nyumbani.

Matatizo yamekuwa makubwa zaidi tangu shule za serikali zilipoanza kutoza ada. Wasichana wengi walitoka katika familia zenye ufukara kiasi kwamba hawamudu kulipa ada na gharama nyingine.

Pia familia nyingi bado zina fikra kwamba ni muhimu zaidi kuwaelimisha watoto wa kiume kuliko watoto wao wa kike.

Serikali imekopa US$ 6.9 milioni kutoka Benki ya Dunia kuwasaidia wasichana wanaotoka katika familia masikini. Fedha hizi zanatumika kwa:

- Kulipa ada, vitabu, vifaa vya kuandikia, usafiri, chakula, huduma za tiba, sare na fedha za matumizi,
- Kutoa ushauri kwa wasichana shuleni,
- Kuendesha semina katika jumuiya.

Wazazi wanaomba msaada wa kulipiwa masomo na walimu wa shule za msingi pamoja na kamati za shule hupendekeza wasichana wenye akili lakini wanaotoka kwenye familia masikini. Mwaka 1997 Tsh. 72,626,000/= zilitumika kuwasaidia wasichana 359 kwa kupitia mpango huu nchini.

Mpango wa Wizara unasema kuwa ifikapo mwaka 2000/1 inataka idadi sawa ya wavulana na wasichana katika shule za sekondari.


**Elimu ya Juu**

Elimu ya juu nchini Tanzania ni pamoja na vyuo vikuu vitano, vyuo vya ufundi vitatu na taasisi nyingine kama vile Taasisi ya Uongozi wa Maendeleo (IDM), Taasisi ya Uongozi wa Fedha (IFM), Taasisi ya Usafirishaji, Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Mipango ya Maendeleo ya Jamii, Kituo cha Mafunzo ya Jamii cha Nyegezi na Taasisi ya Taifa ya Mafunzo ya Ustawi wa Jamii.

Wako zaidi ya wanachuo 12,500 katika elimu ya juu

Tanzania. Takribani theluthi mbili ya wanachuo hawa wako katika vyuo vikuu, moja ya tano katika taasisi mbalimbali na waliobaki wako katika vyuo vya ufundi.

**Uandikishwaji katika Elimu ya Juu 1994-1996**




Mwaka 1995/96 asilimia 15 ya wanachuo 8,076 walikuwa wanawake. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni chuo kikubwa kuliko vyote. Mwaka 1995/96 asilimia 41 ya watu walioomba kwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walikuwa wanawake. Ni asilimia13 ya hao waliokubaliwa ni wanawake. Asilimia 33 ya wanaume ya walioomba walikubaliwa lakini ni asilimia 10 tu ya waliokubaliwa ni wanawake. Zaidi ya theluthi mbili ya wanawake walioomba nafasi ya masomo walitaka kusoma katika kitivo cha Sanaa, asilimia 20 sayansi na asilimia 19 uhandisi. Kwa ujumla, kwa kuwa wanawake wengi hawakukubaliwa, wanawake wanachangia asilimia 10 tu ya wanachuo katika kozi zote isipokuwa sheria (LLB), sayansi (Bsc. Ualimu) na Kitivo cha Biashara.




Katika vyuo vya ufundi asilimia sita tu ya wanachuo ni wanawake mwaka 1994/95. Katika taasisi, asilimia 31 ni wanawake. Katika Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini, Taasisi ya Mafunzo ya Ustawi wa Jamii, zaidi ya nusu ya wanchuo ni wanawake.

Kutokana na uchambuzi huu wa ushiriki wa wanawake na wanaume, kwa jumla mwaka 1995/96 serikali ilitumia Tsh.3,800 milioni kwa elimu ya wanaume katika elimu ya juu ukilinganishwa na Tsh. 683 milioni kwa elimu ya wanawake.

*Jedwali 4.1* **Bajeti ya kawaida kwa Elimu ya Juu 1996/97**

| **Aina** | **Kiasi (Tsh-m)** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ujira na Mishahara | 3,278 | 22% |
| Safari za Nje | 4,472 | 29% |
| Mafunzo na Safari | 520 | 3% |
| Uendeshaji na Ukarabati | 1,121 | 7% |
| Utawala | 1,961 | 13% |
| Vyuo Vikuu | 3840 | 25% |
| Jumla | 15,192 | 100% |

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Elimu ya Juu 1996/97**




Jedwali 4.1 linaonyesha kuwa mwaka 1996/97 serikali ilipanga kutumia Tsh. 15,192m/= kwa Elimu ya juu. Kiasi kikubwa sana kilikuwa ni kwa safari za nje kwa wanachuo. Kiasi kikubwa kinachofuata kilikuwa ni kwa vyuo vikuu. Kiasi cha tatu ni kwa ujira na mishahara.

Serikali inalipa gharama za zaidi wanachuo 1,000 wanaosoma nchi za nje. Mwanachuo anayesoma nchi za nje anaigharamu serikali mara tatu zadi ya yule anayesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kama serikali ingepunguza gharama za kusomesha nje ya nchi kwa nusu, itaweza kulipia wanachuo 1800 zaidi katika vyuo vikuu hapa Tanzania.

Kiasi kikubwa kinatumika kwa 'gharama mahsusi' za Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Kwa pamoja maofisa hawa watatu wanatumia takriban Tsh. Milioni 38. Kiasi hiki cha fedha kinatosha kuwalipia wanachuo 30 wa kike Chuo Kikuu au kuwasomesha wasichana 500 katika shule za sekondari au wasichana 2,600 katika shule za msingi.

**Elimu ya Watu Wazima**

Kati ya mwaka 1970 na 1980 Tanzania ilikuwa na kampeni kubwa za kuwafundisha watu wazima kusoma na kuandika. Mwaka 1977 zaidi ya robo ya watu wazima Tanzania hawakuweza kusoma na kuandika. Mwaka 1986 ni asilimia 10 tu hawakuweza kusoma na kuandika. Mwaka 1992 asilimia ilipanda hadi kufikia 16.

Kuna tofauti kubwa kati ya mikoa kwa idadi ya wanawake na wanaume wasiojua kusoma na kuandika. Lakini katika mikoa yote wako wanawake wengi zaidi kuliko wanaume wasiojua kusoma na kuandika. Mwaka 1992 baada ya kampeni yote asilimia 19 ya wanawake na 13 ya wanaume hawakujua kusoma na kuandika. Wilaya zinawajibika kwa elimu ya watu wazima. Ni vigumu kusema kiasi wanachotumia kwa sababu kila wilaya ina bajeti yake.

**Walimu**

Kiasi kikubwa cha Bajeti ya kawaida kwa elimu kinatumika kwa mishahara. Mwaka 1996/97 takriban asilimia 91 ya bajeti ya kawaida ilitumika kwa mishahara.

Mwaka 1996 kulikuwa na:

- Walimu wa shule za msingi Tanzania 108,874 na asilimia 44 walikuwa wanawake.
- Walimu wa shule za sekondari Tanazania 11,689 na asilimia 26 walikuwa wanawake.
- Wakufunzi ni 1,062 na asilimia 26 ni wanawake.

Kwa jumla asilimia 42 ya walimu 121,625 hapa nchini ni wanawake. Kwa hiyo matumizi zaidi kwa mishahara ya walimu inaishia katika mifuko ya wanaume kuliko mifuko ya wanawake.

Miaka minne iliyopita, serikali ilisitisha ajira ya walimu wapya. Ilifanya hivyo ili kupunguza kiasi kilichotumika kwa mishahara. Katika miaka iliyofuatia, idadi ya walimu ilipungua kwa kuwa wengine walistaafu, walikufa au waliacha uwalimu kwa sababu nyingine. Hii ilimaanisha kuwa madarasa mengi yalikuwa makubwa sana kwa sababu hawakuwepo walimu wa kutosha wa kufundisha.

Mwaka 1998 Wizara ya Elimu na Utamaduni ilisema kuwa ingeajiri walimu wapya 1,700 walimu 1,400 kwa shule za msingi na 330 kwa shule za sekondari. Ilisema kuwa, Wizara itasimamisha kutumia fedha kuwalipa walimu wanaofundisha shule binafsi.

Walimu wengi hawana sifa za kutosha za kufundisha. Kati ya mwaka 1998/99 na 2000/01, Wizara imepanga kufundisha walimu wao 500 wa Daraja A kuwapandisha walimu 200 wa C/B kuwa wa Darasa A na kuwapa walimu 600 wa daraja A vyeti vya Diploma.

**Mapato**

Bajeti ina pande mbili-matumizi na mapato. Kama serikali inataka kutumia zaidi, inabidi iongeze mapato yake.

***Ada***

Njia moja ya serikali kuongeza mapato yake katika sekta ya elimu ni kwa kutoza ada. Ada nyingine hazionyeshwi katika bajeti za Wizara za Elimu. Kwa mfano ada nyingi kwa shule za msingi hukusanywa na shule huko wilayani. Jedwali 4.2 linaonyesha kiasi gani Wizara ya Elimu na Utamaduni ilitaka kukusanya mwaka 1997/98 kwa baadhi ya ada nyingine.

*Jedwali 4.2* **Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa 1997/98 (Tsh. Maelfu)**

| | | |
|---|---|---|
| Shule ya Kimataifa-Arusha | mafunzo & mitihani | 125,409 |
| Shule za Sekondari-Ufundi | mafunzo & mitihani | 885,390 |
| Shule za sekondari Biashara | mafunzo & mitihani | 1,437,660 |
| Shule za Sekondari-Kilimo na malazi | mafunzo, mitihani | 964,820 |
| Elimu Ualimu na malazi | mafunzo, mitihani | 1,024,660 |
| Makumbusho | Viingilio | 23,000 |
| MANTEP | mafunzo & mitihani | 2,600 |
| Barazala mitihani | Ada ya Mitihani | 215,717 |

**Fedha Kutoka kwa Wahisani wa Nje**

Wahisani wengi wa nje hutoa fedha kwa Tanzania kwa ajili ya Elimu. Miaka ya 1970 na ya 1980 zaidi ya asilimia 90 ya fedha kutoka kwa wahisani ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kwa mfano, fedha zilitumika kujenga shule, madarasa na kununua vifaa vya kufundishia. Wakati uchumi ulipokuwa dhaifu, wahisani hawakupenda kutoa fedha zaidi kwa gharama za maendeleo kwa sababu serikali haikuwa na fedha za kutosha kulipia gharama za uendeshaji za kutumia madarasa, shule na

vifaa. Serikali na wahisani wamekubaliana kuwa ni lazima kuhakikisha kuwa shule na madarasa yaliyopo tayari, yanafanya kazi kabla hayajajengwa upya madarasa na shule nyingine.

Fedha kutoka kwa wahisani wa nje zinaongeza mapato ya serikali. Lakini hali hii inaweza kufanya mipango kuwa migumu na kuleta matatizo kama wahisani hawaiambii serikali na hata hawapashani habari kati ya wao kwa wao kile wanachofanya katika sekta hii. Ni hatari kama wahisani hawafanyi kazi pamoja kulingana na mpango mahsusi wa serikali:

- Kutakuwepo na miradi mingi midogo ambayo haisambazwi vizuri nchi nzima,
- Baadhi ya miradi itaendeshwa kwa muda mfupi tu kama wahisani wakiamua kusitisha kutoa fedha au wakazitoa mahali pengine,
- Itakuwa vigumu kwa serikali kuona picha kamili ya kile kinachotokea katika bajeti za elimu,
- Serikali haitakuwa na udhibiti wa bajeti na mipango ya sekta.

Mwaka 1996 Serikali iliamua kufanya mpango wa maendeleo wa sekta ya elimu. Mpango huu unaelezea juu ya kile kinachohitajika na pale ambapo serikali ingependa wahisani wafanye kazi ya pamoja katika miradi. Leo hii wahisani wengi wanatoa fedha kwa gharama za kawaida pamoja na gharama za maendeleo katika bajeti. Vilevile serikali inajaribu kutoa kiasi kidogo cha fedha kwa miradi yote ya maendeleo ili kusiwepo na miradi inayotegemea moja kwa moja wahisani.

Mwaka 1997/98 Tanzania ilikuwa ikipata fedha nyingi kutoka nje kwa ajili ya elimu:-

- Serikali za Denmark, Uholanzi na Norway na Umoja wa nchi za Ulaya kwa pamoja zilitoa Tsh. 805m/= kwa elimu ya msingi,
- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 50m/= kwa elimu ya msingi,
- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 252m/= kwa elimu ya sekondari

kwa wasichana,

- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 300m/= kwa vifaa kwa shule za sekondari,
- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 100m/= kwa Taasisi ya Elimu,
- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 261m/= kwa mipango ya elimu,
- Benki ya Dunia ilitoa Tsh. 50m/= kwa kutekeleza miradi,
- Sweden ilitoa Tsh. 2,047m/= kwa vitabu vya kiada,
- Sweden ilitoa Tsh. 496m/= kwa mafunzo ya walimu,
- Sweden ilitoa Tsh. 1,536m/= kwa elimu ya Watu Wazima,
- Ireland ilitoa Tsh. 191m/= kwa Makumbusho.

Kwa ujumla serikali ilipokea Tsh. 7,244m/= kutoka kwa wahisani wa nje kuisaidia ujenzi wa Mpango wa Maendeleo wa sekta. Serikali iliongeza Tsh. 1,031m/= kwa fedha zake kwa zile zinazotoka nje.

**Ni Nani Mwenye Uwezo wa Maamuzi?**

Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Sehemu wanafanya maamuzi muhimu sana katika serikali.

Idara ya utawala na utumishi katika Wizara ya Elimu na Utamaduni imeajiri wafanyakazi 137. Nusu yao ni wanawake . Lakini ni wanawake 11 tu ndio walio katika nafasi zenye uwezo wa kutoa maamuzi ya muhimu. Nafasi ya juu inayoshikiliwa na mwanamke ni ile ya Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi.

Idara ya Mipango imeajiri wafanyakazi 86. Wafanyakazi 15 tu ni wanawake. Wanawake wawili wako katika nafasi zenye uwezo wa kutoa maamuzi.

Nafasi ya juu inayoshikiliwa na mwanamke ni ya Ofisa Elimu Mwandamizi Daraja la 1.

Idara ya Elimu ya sekondari ina wafanyakazi 38 na kati yao 18 ni wanawake. Wanawake watatu wenye vyeo vya juu ni wa ngazi ya Ofisa Elimu Mwandamizi Mkuu Daraja la 1.

Idara ya Utawala ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ina wafanyakazi 60. Takriban theluthi mbili ni wanawake. Lakini wanapata asilimia 43 ya mishahara yote.

Idara ya Elimu ya Juu ina wafanyakazi 13. Wako wanawake watatu.

### Ni Nini Kitakachosaidia Kufanya Elimu Tanzania Ifanye Kazi Vizuri Zaidi kwa Wavulana na Wasichana?


Tunataka kuona idadi sawa ya wasichana na wavulana katika ngazi zote za elimu. Kwa wasichana na wavulana tunahitaji madarasa zaidi, vitabu vya kiada zaidi na walimu wa kutosha wenye sifa.



*Wasichana na wavulana kupata mazingira mazuri ya kujifunza (pamoja na vifaa vya kujifunzia) ni haki na wala si upendeleo!*

**Kwa elimu ya juu serikali haina budi kuangalia:**


- **Idadi ndogo ya wanawake walio katika elimu ya juu.**
- **Matumizi ya malazi ya wanawake wanachuo ukilinganisha na wale wa kiume.**
- **Wafanyakazi na wanachuo wa kiume wanavyowanyanyasa wanachuo wa kike**



Baadhi ya mambo haya hugharimu fedha ili kuyaweka sawa. Kabla haijatumia fedha zaidi, serikali haina budi kupata mapato zaidi. Baadhi ya njia ambazo serikali inaweza kupata fedha za ziada kutoka ndani ya nchi ni kwa:

**Elimu ya msingi na sekondari, serikali haina budi kuangalia:**

- **Idadi kubwa ya wasichana na wavulana wanaoacha shule.**
- **Wasichana wengi wanaoacha shule kwa sababu ya mimba.**
- **Wavulana wengi walio nje ya shule.**
- **Wazazi wengi wasioweza kumudu kulipa ada ya shule.**



Baadhi ya njia ambazo serikali inaweza kupata fedha za ziada kutoka nje ya nchi ni kwa:

- Kutoa moja ya kumi ya fedha zinazotumika kwa nyumba, samani na usafiri kwa maofisa wa juu zipelekwe katika mfuko wa mafunzo ya wasichana.
- Kuzieleza wilaya ni kiasi gani kitumike kwa vitabu vya kiada na vifaa vingine.
- Kutoza kodi kidogo kwa watu na kampuni zinazotoa vifaa vya elimu na vitu.

- Kutoa kiasi cha fedha kwa elimu ambacho kimepatikana kutoka nchi za nje ambazo zinasema malipo ya riba yawe kidogo kwa mkopo au riba inaweza kulipwa baadaye.
- Kuandaa kongamano la elimu kwa wahisani.
- Kupanga utaratibu ambao shule tajiri zinatoa vitabu vilivyotumika na vifaa vingine kwa shule masikini.

Maoni yako tuma TGNP